SportPesa
TZS. 1,042,431,860
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Askari** adaiwa kujinyonga kwa kutumia mkanda

UKURASA 3




'MBAPPE, HAALAND HAWATAIBADILISHA MANCHESTER UTD'

UKURASA 22


# Nipashe

Alhamisi Machi 17, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • Na. 0580887

www.ippmedia.com

MWANGA W

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 07

LIKE & FOLLOW US

Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akiwa amejipumzisha kizimbani, baada ya kuugua ghafla, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, jana. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Ole Sabaya akaangwa tena kortini

• **Shahidi** adai ni mtu hatari na dikteta, hukumu kesi uhujumu kujulikana Machi 31... *Endelea Uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 11 & 12
**WATANZANIA 'WANAVYOMISI' HULKA, UPENDO WA MAGUFULI**
LEO ni mwaka mmoja umetimia tangu Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli...

UKURASA WA 19
**WANAFUNZI AFRIKA WASIMULIA ADHA FURSA ZA VITA UKRAINE**
IKIWA ni wiki ya tatu tangu mashambulizi ya Russia dhidi ya Ukraine yaibuke, baadhi...

UKURASA WA 19
**SMZ SASA KUKUSANYA MAPATO KIDIJITALI**
SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), kupitia Wakala wa Serikali Mtandao...

## Samia ataja sababu kasi unyanyasaji wa kijinsia

UKURASA 3




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna na Mkurugenzi Mtendaji wa Serikali Mtandao Zanzibar, Said Seif Said, wakibadilishana mikataba baada ya kutiliana saini ya makubaliano ya ushirikiano wa ukusanyaji mapato na malipo ya serikali kwa njia ya kidigitali, jijini Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sharti kuingia nchini cheti chanjo ya corona

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA YAPANIA REKODI MPYA CAF UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea tuzo ya heshima kutoka Nuru Awadh, kwa niaba ya wanawake wenye ulemavu Tanzania kabla ya kuzungumza na makundi mbalimbali ya watu wenye ulemavu, Sauti ya Wanawake wenye Ulemavu (SWAUTA), Shirikisho la Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar (SHIJUWAZA) na Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu SHIVYAWATA, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Shahidi adai Sabaya ni dikteta

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa saba wa utetezi, Watson Mwahomange, katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lenga Ole Sabaya, amedai kwamba kiongozi huyo ni dikteta.

Mwahomange (27) amesema Sabaya alikuwa na uwezo wa kumpiga mtu, kumsweka rumande na kuzuia mtu kupewa dhamana.

Shahidi huyo, ambaye ni mshtakiwa wa tatu katika kesi hiyo, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Dk. Patricia Kisinda wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, wakati akitoa ushahidi katika kesi Na. 27 ya uhujumu uchumi inayomkabili Sabaya na wenzake sita.

Alidai hayo alipoulizwa uhusiano wake na Sabaya akidai kuwa haukuwa mzuri kwa kuwa alikuwa dikteta, hakuwa na furaha kwa kuwa alikuwa anamlazimisha kufanya vitu ambayo hakupenda.

"Sabaya alikuwa anataka ufanye kitu ambacho anataka yeye pia alikuwa anataka uwapo kwa wakati na eneo alipokuwa kwa muda mwafaka. Ninaomba mahakama iniachie huru kwa kuwa matendo yake aliyofanya kwa Mroso ndio yamefanya mimi kuwa hapa.

Pia wakati nikifanya naye nilikuwa na hofu sana kwa kuwa muda wowote hali inaweza kuharibika," alidai.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali, Neema Mbwana, Mwahomange alidai kwamba kwa muda wote aliokuwa akiambatana na Sabaya, aliishi kama mateka kwa kuwa alimlazimisha kufuata matakwa yake.

"Sabaya usipofanya anachotaka, anakupiga na kukuweka mahabusu na huwezi kumkimbia kwa kuwa ni mtu anayetembea sana na huwezi kumkwepa hata nilipojaribu kutoa taarifa ya madhila yaliyonipata ikiwamo kutoa taarifa kwenye ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Arusha (RCO) na Ofisi ya Usalama wa Taifa," alidai.

Alidai kwamba aligundua Sabaya ni mtu hatari mwaka 2020 kutokana na alivyokuwa akimpiga, kumweka rumande na kuzuia kupata dhamana hasa alipomsweka katika vituo vya polisi vikiwamo Sakina, Sekei, Hai na Kituo Kikuu cha Polisi Arusha.

Naye Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ofmedy Mtenga, akimhoji shahidi huyo, alidai Sabaya akimtuma halafu akakaidi kinachotokea ni kupata kipigo au kupelekwa mahabusu.

Akithibitisha hilo katika ushahidi wake, alidai kuwa kabla na baada ya Januari 22, 2021 alipigwa zaidi ya mara tano bila kuwa na kosa kwa kuwa alitaka afanye anachotaka.

Pia akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tersila Gervas, shahidi huyo alidai kwamba alipigiwa simu na Sylvester Nyegu, akimweleza kuwa mkuu ambaye ni Sabaya anamwita katika Hoteli ya Point Zone.

Alidai kwamba Nyegu alikuwa msaidizi binafsi wa Sabaya na alipokea mikoba hiyo kutoka kwa Lameck baada ya kuacha kuwa msaidizi mwaka 2020.

Mwahomange alidai kuwa alifungwa pingu na kuwekwa kwenye gari kisha kupelekwa kwa mfanyabiashara Francis Mroso bila yeye kuwaeleza. Alidai kuwa wakati wanatoka Point Zone kwenda kwa Mrosso, gari aina ya VX Masai lilikuwa likiendeshwa na dereva anayetambulika kwa jina la Shukuru.

Ushahidi wa utetezi ulifungwa rasmi jana baada ya shahidi wa nane mshtakiwa wa saba, Nathan Msuya (31), kutoa ushahidi wake huku akidai kwamba hakuhusika kuunda genge la uhalifu na kutakatisha fedha Sh. milioni 90 kama ilivyodaiwa mahakamani mashahidi wa Jamhuri.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Edmund Ngemela, alidai kwamba anafanya shughuli ya ufugaji wa kuku na nguruwe.

Baada ya kumalizika kutolewa kwa ushahidi huo, Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, aliomba mahakama kufunga ushahidi kwa upande wa utetezi na kuomba mahakama kuwaruhusu kufanya majumuisho ya mwisho kwa pamoja ndani ya siku 14 kuanzia jana.

Wakili wa Serikali Mtenga, aliunga mkono kwa kudai kuwa muda huo unawatosha kufanya majumuisho ya mwisho kwa njia ya maandishi ambayo yataambatana na nyaraka ambazo zitaisaidia mahakama kutoa hukumu.

Hakimu Kisinda alisema mahakama imekubali maombi hayo na kitaka yawasilishwe Machi 31, mwaka na siku hiyo mahakama itatangaza tarehe ya hukumu.

# Sharti kuingia nchini cheti chanjo corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imelegeza masharti kwa wasafiri wanaotoka nje ya nchi na kuanzia leo wataingia nchini bila kuwa na cheti cha kupima maambukizo ya UVIKO-19 badala yake wataonyesha cheti cha chanjo inayotambulika na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Aidha, serikali imeruhusu wazazi ambao watahitaji watoto walio chini ya miaka 18 kupatiwa chanjo ya UVIKO-19, kuomba kibali kwa maandishi.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu miaka miwili ya mapambano dhidi ya UVIKO-19.

"Mtakumbuka Machi 16, 2020 ndipo taifa letu lilipata kisa cha kwanza cha mgonjwa wa virusi vya corona katika mkoa wa Arusha hadi leo hii ni miaka miwili ya mapambano haya.

"Serikali inalegeza masharti kwa wasafiri wanaoingia nchini ambao wamekamilisha dozi ya chanjo ya UVIKO-19 hivyo kuanzia kesho (leo) wanaondolewa hitaji la kuwa na cheti cha kipimo cha kuthibitisha kutokuwa na maambukizi (Negative RT - PCR certificate) kilichokuwa kikihitajika hapo awali," alisema Ummy.

Alisema masharti hayo na mengine yataainishwa kwenye mwongozo wa wasafiri ambao utakuwa ukibadilika kulingana na mwenendo wa maambukizi ya ugonjwa huo nchini na duniani kwa ujumla.

"Pia huduma za kipimo cha haraka (COVID-19 Rapid Antigen Test) zitaanza kutolewa ndani ya wiki moja katika vituo mbalimbali vya huduma za afya nchini," alisema.

Akizungumzia kuhusu kutoa chanjo kwa watu wenye umri chini ya miaka 18, alisema serikali imeamua kutoa ruhusa kwa mzazi yeyote mwenye mtoto ambaye atahitaji kupata chanjo kuomba kibali kwa njia ya maandishi.

"Kwa mzazi yeyote ambaye ataona kuwa kuna umuhimu wa mtoto wake kupata chanjo tunamruhusu kuandika kwa maandishi kuji - 'commit' ili mtoto kupewa kibali cha kupata chanjo. Hivi sasa kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wazazi ambao watoto wao wanasoma bweni kuhitaji chanjo na hata wale ambao wako katika shule za kimataifa," alisema Ummy.

Kuhusu hali ya ugonjwa huo nchini, alisema hadi kufikia juzi watu 33,789 wamethibitika kuwa na maambukizi ya UVIKO - 19 huku watu 803 wakipoteza maisha.

Kadhalika, alisema serikali imeendelea kuikinga jamii kwa kuwezesha upatikanaji wa chanjo ya UVIKO-19 nchini na hadi Machi 12, watu 2,820,545 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea, wamepata chanjo kamili dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema idadi hiyo ni sawa na asilimia 9.17 ya Watanzania 30,740,928 wenye umri wa miaka 18 na kuendelea ambao wanakidhi vigezo vya kuchanja.

"Idadi hii bado hairidhishi kwa kuwa ili kufikia kinga ya jamii tunapaswa kuchanja angalau asilimia 70 ya watu wenye umri wa miaka 18 na kuendelea," alisema.

Akizungumzia hali ya UVIKO-19 katika wimbi la nne nchini kwa sasa, waziri huyo alisema limepungua kwa kiasi kikubwa tangu lilipoanza mwanzoni mwa mwezi Desemba 2021. Alisema wakati huo watu 4,285 walithibitika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

"Kwa Januari 2022 wagonjwa waliothibitika walikuwa 2,737 na kwa kipindi cha Februari 2022, wagonjwa 401 walithibitika kupata maambukizi ya ugonjwa huo.

"Kupungua kwa maambukizi mapya ya ugonjwa wa COVID-19 kumeripotiwa pia katika baadhi ya nchi duniani huku kukiambatana na kulegezwa kwa masharti ya kuzuia kusambaa kwa maambukizi," alisema.

Hata hivyo, alisema ndani ya wiki hii kumeripotiwa taarifa ambazo bado hazijathibitishwa na WHO kuhusu kuibuka kwa aina mpya ya kirusi cha UVIKO-19 China, Korea Kusini na Japan.

Alisema, Wizara ya Afya inaendelea kuwasiliana na WHO kuhusu suala hilo sambamba na kuendelea kuimarisha ukaguzi na ufuatiliaji wa wasafiri wanaoingia nchini.

# Samia ataja sababu kasi unyanyasaji kijinsia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema tatizo la ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto ni kubwa nchini na linatokana na kuporomoko kwa maadili huku akiwataka wazazi kupaza sauti na kufichua wanaofanya vitendo hivyo.

Pia, amesema serikali itahakikisha inashughulikia kero zinazowakabili watu wenye ulemavu na kwamba suala la kuanzishwa kwa mfuko kwa ajili yao lipo kwenye hatua za mwisho.

Aliagiza kutambuliwa mapema watoto wenye ulemavu wanapozaliwa na aina za ulemavu wao ili kuandaa afua zao.

Rais Samia aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na watu wenye ulemavu, Ikulu ya Chamwino, mjini Dodoma.

"Tatizo la ukatili wa kijinsia ni kubwa sana ndani ya nchi yetu na nilikuwa naongea na viongozi wa dini hapa kuna maporomoko ya maadili kwamba watu wameishiwa hawa maadili, lakini kubwa ni kutomtambua Mungu."

"Kama unamtambua Mungu na unamjua Mungu unajua ndiyo aliyekutengeneza wewe amemtengeneza huyu huwezi kwenda na kufanya ukatili dhidi yake awe mzima au mwenye ulemavu."

"Ndugu zangu, viongozi wa dini tulifanyie kazi hili la unyanyasaji wa wanawake na watoto, jingine wakati nazungumza Rufiji na wanawake, nikazungumza juzi Zanzibar na wanawake, kama kweli hatulitaki hili na linatuchukiza tutapaza sauti tuseme na tutakuja na mipango tuiambie serikali yetu kwamba hili linatukwaza," alisema.

Aliwataka kupaza sauti kusema na kuwafichua wanaofanya vitendo hivyo.

"Lakini cha ajabu likitokea mwanamke uliyezaa huyo mtoto aliyefanya hivyo unaficha, wa kwanza kwenda kunong'ona mstiriane...ooh yaishe, matokeo yake huyo nunda anakwenda kufanya kwa mwingine na kwa mwingine, kwa hiyo wanawake tupige moyo konde."

"Niliangalia clip moja kama sio Uingereza, Marekani mtoto anaiba kwenye supermarket akatolewa kwenye kamera wakasema atakayemuona amlete basi kazurura huko siku kadhaa karudi kwa mama yake alivyoingia ndani mama kapiga simu polisi lile nunda limekuja, njooni," alisisitiza kwa mfano huo.

"Huyu mama anafuata sheria za nchi, anaishi kwa kufuata sheria sasa watoto wetu tunaona uchungu sana wakifanya makosa hata wangu, wakifanya makosa naona uchungu sana, natamani kosa lile ligeuzwe, kosa lile asingefanya wako angefanya wa mwenzio ungelibebaje? Mzazi mwenzio anajihisije? Nadhani sisi wazazi tuanze sisi kuchangamka."

Rais Samia alisema wanaume wanatumia silaha zao kuharibu watoto wengine wa kiume, jamii inakwenda wapi, inaelekea wapi? "Hili jambo kama linatuudhi badala ya kukaa kwenye mikutano na mihadhara hivi tuanze kufanyia kazi ndani ya familia, tukianza huko suala la maadili likifika ngazi ya taifa litakuwa limefanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa na kupungua, naomba hili litukere na tukalifanyie kazi huko."

Kuhusu vikwazo vya watu wenye ulemavu, Rais Samia alisema serikali imekuwa ikitatua kupitia sera, sheria na mikataba mbalimbali ya kimataifa.

"Kundi lenu ni muhimu sana ambalo linakadiriwa kuwa na asilimia 5.8 ya Watanzania wote wanaokadiriwa kuwa milioni 60, sote tunatambua kundi hili lina changamoto na mahitaji mahsusi ambayo yanatulazimu serikali na jamii kwa ujumla kuweka mipango mikakati mahsusi kwa ajili ya kukidhi mahitaji hayo," alisema.

Alisema vikwazo vinavyowakabili watu wenye ulemavu vipo kwenye makundi mawili makubwa, zipo za kiumaumbile na za kijamii namna inavyowatazama na upatikanaji wa huduma.

Alisema kutokuwapo kwa mifumo mahsusi ya uchambuzi wa mapema wa aina mbalimbali za ulemavu kunasababisha kutopata huduma mapema.

"Nakumbuka ndugu zangu wakati mimi naleta shangazi zenu, wajomba na ndugu zenu ukishajifungua kuna daktari maalum anapita kukagua mtoto anamkagua viungo vyote na kama kuna tatizo anaanza kushughulikiwa mapema sasa sijui kama hili linaendelea? Hili lifanyiwe kazi kuwapo na utambuzi wa mapema," alisisitiza.

Kuhusu umaskini na utegemezi wa kiuchumi, Rais Samia alisema serikali inalitambua na inalifanyia kazi kwa kuchukua hatua kunyanyua maisha ya watu hao kupitia mipango mbalimbali ili waishi kwa kupata mahitaji yao ya msingi.

"Kuanzishwa kwa mfuko wa taifa wa watu wenye ulemavu, upo hatua za mwisho linaletwa kwenye vikao mbalimbali vya serikali ili lithibithishwe na kuanza kazi," alisema.

**MAMBO 15 SHIVYAWATA**

Awali, akisoma risala ya watu wenye ulemavu nchini, Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Ernest Kimaya, aliwasilisha mambo 15 kwa Rais wanayohitaji na yanayowakabili ikiwamo ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto wenye ulemavu, uhaba wa vifaa tiba bandika kwenye hospitali, visaidizi, ajira na ushirikishaji mambo ya kijamii.

Aliomba kupatiwa majengo ya serikali yatakayotumika kama Ofisi zao katika Jiji la Dar es salaam, kutanua wigo wa uteuzi ili kuongeza uwakilishi wa watu hao kwenye ngazi za maamuzi.

## Askari polisi adaiwa kujinyonga kwa mkanda

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ASKARI Polisi Novatus Kalambo anadaiwa kufariki dunia baada ya kujinyonga kwa mkanda wa suruali yake akiwa nyumbani kwake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (SACP) Ulrich Matei, alisema jana kuwa chanzo cha kifo chake bado hakijafahamika na kwamba Kalambo alikuwa akisumbuliwa na maradhi ya moyo.

Alisema Kalambo alifariki dunia juzi majira ya saa 11 jioni nyumbani kwake eneo la Mwambene jijini Mbeya baada ya kuingia nyumbani na kujifungia chumbani kwake bila familia yake kujua alichokuwa akikifanya.

"Kalambo alikuwa askari ambaye anafanya shughuli za kawaida katika Kituo Kikuu cha Polisi Mbeya. Kutokana na tatizo la moyo, alipata likizo ili akatibiwe. Huenda ugonjwa ulimsababishia mawazo na kuchukua uamuzi wa kujinyonga, "alisema Kamanda Matei.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Matei aliwashauri watumishi wa Jeshi la Polisi kuwa pindi wanapopitia nyakati ngumu katika maisha ni vyema kuwashirikisha na kuomba ushauri kwa watu wao wa karibu au watalaam wa saikolojia ili kupata faraja.

Alisema mwili wa marehemu ulisafirishwa jana jioni kwenda mkoani Rukwa kwa ajili ya mazishi na kwamba atazikwa bila heshima za kijeshi kwa sababu alijinyonga.

Diwani wa Mwambene, Lucas Mwampiki, alisema Kalambo alikuwa likizo akipata matibabu ya moyo na kwamba baada ya afya yake kuimarika alikuwa na utaratibu wa jioni kutembea kwa jamaa na marafiki.

Alisema Machi 15, majira ya saa 9:00 alasiri, alipita mtaani akirejea kutoka kwenye matembezi yake na ndipo aliingia ndani na kuchukua uamuzi wa kujinyonga.

Diwani Mwampiki alisema familia ilishtuka baada ya kugundua mlango wa chumba chake umefungwa na baada ya kufanya jitihada ndipo wakagundua amejifunga mkanda shingoni akiwa amelala.


## NOTISI/TANGAZO

MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MWANZA | ABBAS HAMAD ISSA | NYUMBA | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 31/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | PENDO JEREMIAH HANGO | NYUMBA | JEREMIAH EFRAIM | KIBADA | 31/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | GRACE ATILIO MBOKA | NYUMBA | JOEL BUTA CHAULA | KUNDUCHI-MTONGANI | 5/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | SUNNY KEWAL SINGH | NYUMBA | BERNARD PATRICK MABINZA | MBEZI MSAKUZI | 6/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | JOHN NYANGAKA MAKANG'A | NYUMBA | JOHN NYANGAKA MAKANG'A | TABATA | 8/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | NEEMA DAVID MUSHI | NYUMBA | ANTIDIUS MATHIAS KARUMUNA | KIMARA MAVURUNZA | 6/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | ERICK MPENDAEL MNDEME | NYUMBA | ERICK MPENDAELI MNDEME | KWEMBE MPAKANI | 12/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | NIGANILE NELSONI MWAKAJOKA | NYUMBA | NIGANILE NELSONI MWAKAJOKA | GOBA KINZUDI | 12/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | OMAR ISSA NGALGAL | NYUMBA | OMARY ISSA NGALGAL | VIWEGE- MAJOHE | 13/04/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | NEEMA ARON URIO | NYUMBA | OMARI ATHUMAN MKINDI | KIGAMBONI VIJIBWENI | 31/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| HEAD OFFICE | EVELYNE KASHUSHURA MHINA | GARI TOYOTA SPACIO NO.T973 CKU | EVELYNE KASHUSHURA MHINA | CHANG'OMBE TEMEKE | 31/03/2022 SAA04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MASHARTI YA MNADA | | | | | |
| 1 | Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba ,Kiwanja au Gari ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14. | | | | |
| 2 | Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo yaawali,hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa. | | | | |
| 3 | Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0752360133/0765999000/0715363537/0652691275 | | | | |
| 4 | Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote. | | | | |






HONGERA

BODI YA WAKURUGENZI NA WAFANYAKAZI WA BINGWA LABORATORIES LTD WATENGENEZAJI WA BIDHAA ZA EMINA TUNAKUPONGEZA MH. RAIS SAMIA SULUHU HASSAN KWA KUTIMIZA MWAKA MMOJA MADARAKANI NA KUIONGOZA NCHI YETU VIZURI, MUNGU AKULINDE....*Kazi iendelee!*

+255 745 215 253 www.emina.co.tz emina_east_africa

# Serikali yashtukia uzalishaji vinywaji bandia, yakosa tril. 1.2/- kila mwaka

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeagiza wazalishaji wa bidhaa mbalimbali nchini kurasimisha bidhaa zao na kutoa onyo kwa watakaoendelea kwenda kinyume cha agizo hilo.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alitoa agizo hilo jana alipozungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam baada ya kumalizika kwa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara katika Kiwanda cha Konyagi (TDL).

Alisema kuwa wazalishaji watakaozalisha bidhaa zisizorasimishwa, watachukuliwa hatua za kisheria kwa kuwa wamekuwa wakiikosesha serikali mapato.

"Sisi kama wizara tutahakikisha wale ambao wanazalisha nje ya utaratibu tutawasaidia warasimishe lakini wale watakaoendelea na uzalishaji wa bidhaa bandia watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kukamata na kuharibu bidhaa hizo zinazouzwa kwa njia ya panya.

"Tuna utaratibu wa kusimamia wazalishaji ili wazalishe kwa tija na wasaidie uchumi wa nchi," alisema Naibu Waziri Kigahe. David Kihenzile, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara na Mbunge wa Mufindi Kusini , alisema kuwa kamati hiyo ipo kwenye ziara ya kutembelea viwanda na taasisi mbalimbali zinazojihusisha na biashara na mazingira na kwamba walizuru kwenye kiwanda cha TDL kwa ajili ya kuona wazalishaji na kero zao.

Alisema kamati hiyo imesikia kilio cha wazalishaji hao kuwa bidhaa bandia zinazouzwa mitaani zimekuwa kikwazo kwenye bidhaa zao. Alisema wamewasikia TDL wakidai kuwa takribani asilimia 55 ya bidhaa zinazouzwa mitaani ni bandia.

"Kama kweli hali ipo hivyo, ni hatari na kwamba serikali inakosa karibia Sh. trilioni 1.2 za kodi kwa mwaka. Ukisikia hivyo unawaza kiasi hicho kingejenga barabara ngapi, vituo vya afya vingapi, tungepata dawa kiasi gani? Kwa hiyo unaona madhara yake," alisema Kihenzile. Alibainisha kuwa kamati hiyo imemwomba waziri alichukue kwa uzito suala hilo na serikali iwadhibiti wazalishaji wa bidhaa bandia.

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa TDL, Mesiya Mwangoka, aliomba serikali kutengeneza adhabu kali zaidi ili wale wote wanaohusika na kutengeneza bidhaa bandia wasiendelee kufanya biashara hiyo.

"Tunaomba serikali kutunga adhabu kali zaidi kwani adhabu za sasa hivi zinamwezesha yule anayetengeneza bidhaa bandia kuendelea na biashara yake, faini zake ni ndogo sana, unakuta mtu anazalisha bidhaa bandia ya Sh. milioni mia mbili, faini yake analipa Sh. milioni mbili, lazima aendelee kuzalisha kwa sababu haoni hasara kwa kuwa adhabu anayopewa ni ndogo sana na haimfanyi yeye kuvunja ile biashara," alifafanua Mwangoka. "Tumefanya utafiti mwaka jana sisi kama TDL kupitia wakaguzi, inaonyesha serikali inapoteza kwa mwaka takribani Sh. trilioni 1.2 kutokana na bidhaa bandia zilizopo mtaani," alisema Meseia.

Lengo la kamati kuzuru TDL ni kuangalia namna ya kutatua tatizo la bidhaa bandia mitaani na kujiridhisha kuhusu mikakati ya serikali kusaidia wawekezaji kwa kudhibiti bidhaa bandia .

Alisema kamati hiyo imesikia kilio cha wazalishaji hao kuwa bidhaa bandia zinazouzwa mitaani zimekuwa kikwazo kwenye biashara zao.

Alisema kuwa TDL inajitahidi kupanua soko la uzalishaji wa mvinyo na ina mpango wa kuongeza nguvu kwenye kilimo cha zabibu lakini kikwazo kikubwa kimekuwa wazalishaji wa bidhaa bandia.

# Mpango ataka jitihada kupinga ukatili

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewaagiza viongozi wa dini na serikali kuongeza jitihada katika kupiga vita ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake, ili kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amekubali kuwa kinara wa mapambano hayo.

Alitoa agizo hilo jana katika Kijiji cha Magara, Wilaya ya Babati baada ya kuzindua daraja la Magara lenye urefu wa mita 84.

"Mkuu wa Mkoa ukapaze sauti yako kwa kupinga ukatili kwa kuwa jambo hili linatutia aibu. Inawezekanaje miaka 60 ya uhuru kuendelea kufanya ukeketaji?" Alihoji.

Makamu wa Rais alisema viongozi wa dini wakalikemee jambo hilo kwa kuwa mila zingine ni za kuachana nazo, ili watoto wasome na kuwa madaktari, wahandisi au walimu kwa ajili ya ustawi wa taifa.

Dk. Mpango alisema watoto wa kike wakinyanyasika toka utotoni watakuwa hawajiamini, watashindwa kuwa viongozi wakubwa kama Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu.

Pia Dk. Mpango alimwagiza Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, kuhakikisha wizara inafanya utafiti wa kutosha ili zikijengwa barabara zidumu kwa muda mrefu kama ambavyo limejengwa kwa viwango daraja la Magara.

"Wabunge wawabane mawaziri wawajengee barabara zinazodumu kwa miaka mingi hadi 200. Naona daraja hili limejengwa kwa ubora. Sitaki wananchi waje waseme nimewadanganya," alisisitiza Dk. Mpango.

Makamu wa Rais alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi walitunze daraja hilo ili na watoto wao waweze kufaidi matunda yake.

Kiongozi huyo barabara ambayo aliipigia chapuo ni kutoka daraja la Magara lililoko Wilaya ya Babati hadi Mbulu yenye urefu wa kilometa 50 na ile inayotoka Hydom/Mbulu hadi Sibiti mkoani Simiyu yenye urefu wa kilometa 461.

Akizungumzia ujenzi wa daraja la Magara, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Rogatus Matibila, alisema lilianza kutumika Februari, 2020 na kwamba lilianza kujengwa Septemba 11, 2019 kwa gharama ya Sh. bilioni 11.2 na kwamba zitajengwa kilomita 50 kwa kiwango cha lami hadi Mbulu.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, daraja hilo lina urefu wa mita 84 na kwamba kilometa 3.8 ni za lami na kilometa 1.4 kiwango cha changarawe, na kwamba linaweza kupitisha magari yenye tani 56 na kudumu kwa miaka 100.

Aidha, alisema adha walizozipata watumiaji wa daraja hilo ni wakati mvua zinanyesha magari yalizama, na

Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Suleiman Jafo, alipopewa nafasi mbele ya Makamu wa Rais, alithibitisha gari lake liliwahi kuzama kwenye mto huo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
SERA, BUNGE, URATIBU, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU
WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI (OSHA)

KUMBUKIZI YA MWAKA MMOJA YA KIFO CHA DKT. JOHN POMBE MAGUFULI



Bodi ya Usimamizi, Menejimenti na Wafanyakazi wa **Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA),** tunaungana na **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan** na Watanzania wote katika kumbukumbu ya Mwaka Mmoja ya kifo cha **Dkt John Pombe Magufuli** Rais wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichotokea Machi 17, 2021.

**Tutaendelea kukuenzi kwa vitendo kwa kulinda nguvu kazi kwa maendeleo endelevu ya Taifa**

*"Usalama na Afya Mahali pa kazi huongeza tija" OSHA inasimamia hilo*

Occupational Safety and Health Authority
osha_tanzania_official
TanzaniaOsha
Osha online TV
SIMU YA BURE: 0800110091/2

Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA),
P.O Box 519, DAR ES SALAAM
Simu Na: +255 (0)22 2760548/276055
Nukushi Na: (022) 27605 Barua pepe: info@osha.go.tz



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS
MUUNGANO NA MAZINGIRA



1959 - 2021

KUMBUKIZI YA MWAKA MMOJA WA HAYATI
DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI

Ofisi ya Makamu wa Rais inaungana na Watanzania wote katika kumkumbuka aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati **Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.** Ofisi inaenzi mchango wake katika kudumisha Muungano na Usimamizi wa Mazingira nchini.

**Tunamuombea aendelee kupumzika kwa amani**

# MATANGAZO


World Health Organization

## TERMS OF REFERENCE

**INDIVIDUAL CONSULTANT – Data Officer**
**Position Description:**

| | |
|---|---|
| Position Number: | N/A |
| Position Title: | Data Officer - 1posts. |
| Grade and Step: | NOB-01 |
| Unit/Team: | UHC - CND |
| Major Office: | WCO Tanzania |
| Duty Station: | Dar es Salaam |
| Organization: | WHO |
| Nature of Position: | SSA |
| Date Classified: | |
| CCOG Code: | |
| First Level Supervisor: | WHO IVD Focal Person |
| Second Level Supervisor: | WHO Representative |

**1. Rationale**

**Purpose of the Consultant:**
The outbreak of wild poliovirus type 1 in Malawi genetically linked to WPV1 that was detected in Pakistan; Sindh province in October 2019 is a serious concern and underscores the importance of prioritizing polio immunization activities. Until polio is fully eradicated, all countries remain at risk of importation and must maintain high vaccination coverage to protect all children from polio.

WHO and partners are supporting health authorities in Malawi and neighboring countries of Zambia, Mozambique, and Tanzania to conduct a thorough assessment of the situation and begin urgent immunization activities in the subregion to mitigate any risk of spread. Surveillance measures are also being expanded in all countries neighboring Malawi to detect any other potential undetected transmission.

Data management for VPDs is very important in order to continue with routine immunization and strengthen vaccine-preventable diseases surveillance. The data manager will support with planning, coordination, and implementation of data harmonization meetings (IVD, laboratory, IDSR, DHIS), timely reporting of data to different levels of the organization, analysis, feedback to sub national level, and preparations of mitigation plans. (Detailed ToR is available).

**Scope and Methodology**
Under the general guidance and supervision of the WHO IVD Focal Person, and overall supervision of the WHO Representative (WR), the incumbent will provide technical support to the Ministry of Health, Immunization and Vaccine Development program for data management, the incumbent will perform the following:

**Summary of Assigned Duties:**
1. To support the MoHCDGEC IVD program in developing annual plans for data management (collection, storage, analysis and interpretation).
2. Support and ensure development of a comprehensive chronogram for implementation of immunization data improvement activities.
3. Support MoHCDGEC IVD data manager to ensure coordination and implementation of data harmonization meetings (IVD, laboratory, IDSR, DHIS).
4. Support MoHCDGEC IVD data manager to ensure the compilation of Risk assessment data for polio and measles at national level and prepare mitigation plan.
5. Support a Support MoHCDGEC IVD data manager to ensure data management guidelines and data collection tools and other materials have been developed, printed and distributed to lower level.
6. Support MoHCDGEC IVD data manager to Support and ensure data management training and supervision plans at sub national level have been well conducted as per plan.
7. Support MoHCDGEC IVD data manager to Support and ensure quality implementation of sentinel surveillance sites data management.
8. Support MoHCDGEC IVD data manager to Support and ensure quality monitoring of data quarterly (Data cleaning and harmonization) and provide feedback to the sub-national level for correction.
9. Support MoHCDGEC IVD data manager to Compilation and merging of the databases received from the sub-national level and report to WHO IST as per schedule
10. Support MoHCDGEC IVD data manager to Analyse data on a weekly/monthly and share with programme officers
11. Support MoHCDGEC IVD data manager to monitor the completeness and timeliness of datasets
12. Support MoHCDGEC IVD data manager to collate and submit JRF before the end of March of each year
13. Support MoHCDGEC IVD data manager to provide weekly/monthly feedback to sub-national levels
14. Support MoHCDGEC IVD data manager to participate and provide data in all programme reviews and surveys
15. Perform any other duties assigned by the WHO representative.

**Technical Supervision**

Objectives of the Review
The mission of WHO's Health Emergencies Programme (The Programme) in responding to Polio Outbreak is to assist the country's response and, to coordinate international action, to promptly respond to Polio to stop the transmission and recover from PolioOutbreak.

**2. Specific Requirements**

**LANGUAGE:**
**Essential:** Excellent knowledge of English.
**Desirable:** Working knowledge of Swahili, Knowledge of French or other UN languages is an asset.

**EDUCATION:**
**Essential:** Bachelor's Degree or Advanced diploma in Computer Science, statistics or related field.

**Desirable:** Masters university degree in, IT or related field.

**Experience:**
Essential: A minimum of 3+ years' experience in data management or analysis
Desirable: Prior humanitarian working experience at field level in the management of disease outbreak or ant public health emergency

**SKILLS AND COMPETENCIES**
1. Ability to decipher and organize large amounts of data.
2. An analytical mindset with superb communication and problem-solving skills.
3. Knowledge of Epi info and GIS will be an added advantage.
4. Ability to work under pressure to make decisions, elaborate strategies, and organize priorities.
5. Ability to coordinate activities and undertake multitasks.
6. Strong analytical skills and good judgment.
7. Sense of prioritization and attention to detail.
8. Ability to liaise with people at all levels and proactively search for information.
9. Self-motivated, flexible, and able to innovate.
10. Professional commitment.
11. Ability to write in a clear and concise manner, and to present information.
12. Ability to work in a stressful context and under a tight deadline
13. Ability to work in an international and multi-cultural environment

**WHO COMPETENCIES REQUIRED**
1. Producing results
2. Knowing and managing yourself
3. Communication in a credible and effective way
4. Fostering integration and teamwork
5. Building and promoting partnership
6. Respecting and promoting individual and cultural differences

**Other Skills (e.g. IT):**

**Excellent knowledge of Microsoft Office applications.**
1. Good knowledge in computer and Microsoft applications (Excel, Word, Power point)
2. Working knowledge of online data collection applications, statistical analysis packages (Stata, SPSS, etc).
3. Working knowledge of GIS mapping software (or similar) would be an asset

**PLACE OF ASSIGNMENT**
1. The Data officer will be stationed at Dar es Salaam Country Office, Tanzania.

**3. TIMELINE AND REPORTING**

**Duration**
1. The contract will be for (six (06) months

**Salary**

Grade: NOB /ICS 9 payable on monthly bases.

**APPLICATION PROCEDURE**
- The interested candidates should address an application comprising of a detailed Curriculum Vitae, Application letter, copies of certificates/diplomas/degrees and testimonials via the following link: **https://careers.who.int/careersection/ex/jobdetail.ftl?job=2202265&tz=GMT%2B03%3A00&tzname=Africa%2FNairobi**
- Deadline for submission of applications is Friday, 30th March 2022
- Qualified Females and disabled peoples are highly encouraged to apply.

**N.B.** Only shortlisted candidates will be contacted.

World Health Organization

## TERMS OF REFERENCE

**INDIVIDUAL CONSULTANT - TO ASSIST WITH RESPONSE TO POLIO OUTBREAK IN TANZANIA FOLLOWING MALAWI WPV1 OUTBREAK AND ENSURE STRENGTHENING OF SURVEILLANCE.**

Position Description:

| | |
|---|---|
| Position Number: | N/A |
| Position Title: | Individual Consultant - 7posts. |
| Grade and Step: | NOC-01 |
| Unit/Team: | UHC - CND |
| Major Office: | WCO Tanzania |
| Duty Station: | Dar es Salaam |
| Organization: | WHO |
| Nature of Position: | SSA |
| Date Classified: | |
| CCOG Code: | |
| First Level Supervisor: | WHO IVD Focal Person |
| Second Level Supervisor: | WHO Representative |

**Background:**
Tanzania was certified as Polio- Free country by ARCC in November 2015 with the last Polio cases traced back to July 1996. The country has achieved and maintained standard AFP surveillance performance indicators and ensured key performance indicators. Surveillance performance varies slightly between regions (1st administrative level) but varies significantly among councils (2nd Administrative level).

The outbreak of Wild poliovirus type 1 in Malawi genetically linked to WPV1 that was detected in Pakistan's Sindh province in October 2019 is a serious concern and underscores the importance of prioritizing polio immunization activities. Until polio is fully eradicated, all countries remain at risk of importation and must maintain high vaccination coverage to protect all children from polio.
WHO and partners are supporting health authorities in Malawi and neighbouring countries of Zambia, Mozambique and Tanzania to conduct a thorough assessment of the situation and begin urgent immunization activities in the subregion to mitigate any risk of spread. Surveillance measures are also being expanded in all countries neighboring Malawi to detect any other potential undetected transmission.

Consequently, this ToR is put together for the consultant to support the intensification of surveillance, routine immunization and supplementary immunization campaign.

**1. Purpose of the Position**
Consultants with experience in country support to assist countries at risk of polio outbreak from neighboring countries and to assist with intensification of surveillance, routine immunization and immunization campaign. The consultants with experience in strengthening AFP surveillance, routine immunization and conducting MR, IPV, OPV and integrated campaigns.
The consultant will assist with improving quality of immunization campaigns and surveillance for poliovirus for eradication of poliomyelitis due to wild or vaccine related poliovirus in case it happens in Tanzania and to detect and interrupt any new outbreaks due to wild or vaccine-derived polioviruses more rapidly.

**2. Objectives of the Programme and of the immediate Strategic Objective**
- To eradicate poliomyelitis due to wild or vaccine related poliovirus. Complete the interruption of wild poliovirus transmission globally, and more rapidly detect and interrupt any new outbreaks due to wild or vaccine-derived polioviruses.

**3. Organizational context**

Under the direct supervision of the WHO Polio Team Leader, the incumbent will perform the required duties within the framework of WHO program and policy documents.

**Summary of Assigned Duties**
1. Monitor progress and identify risks in regions and districts assigned.
2. Promote activities to enhance Acute Flaccid Paralysis (AFP) surveillance, including rapid surveillance assessments, development of action plans to improve surveillance, evaluation of the impact of these plans, and training/orientation of national and sub-national staff.
3. Develop and manage approaches in assigned regions that can achieve polio eradication while contributing to strengthening routine immunization systems.
4. Assist with preparations for Polio immunization campaign readiness.
5. Provide technical guidance for coordination and planning of Supplementary Immunization Activities (SIA) planning in outbreak-affected regions as well as SIA activities to reduce vulnerability in countries at high risk of outbreaks.
6. Evaluate and document outbreak response activities to ensure that all lessons learned are effectively incorporated into current best practices.
7. Submit a weekly and monthly report.
8. Perform other duties, as may be requested by the supervisor.

**Major output from consultant:**
- Produce a summary report with all surveillance indicators monthly and provide feedback to regions and districts.
- Produce mission reports after each field surveillance visit and submit to IVD Team leader.
- Provide a list of surveillance priority sites and a matrix for supportive supervision.
- Produce report of regional review meetings and comprehensive report of performance quarterly to IVD Team leader.
- Produce a report of the status of preparations for the Polio campaign and implementation.

**Consultancy Requirements:**

Education:
The consultant should normally have the following qualifications:
- First degree in medical/health field, a degree in Public Health, Epidemiology, Health Services Management or related field.

Exprience:
- At least 5 years working in the health sector in Tanzania.

Skills (e.g. IT)
- Good knowledge in computer and Microsoft applications (Excel, Word, Power point)
- Good understanding of the Tanzania health system;
- Good understanding of immunization services ;
- Experience in working as National STOP Polio team
- Considerable experience in Vaccine-preventable diseases surveillance especially AFP and measles case-based surveillance.
- Experience in working with multiple health sector stakeholders;
- Excellent writing and presentation skills;
- Indepeth understanding of the Expanded Program on Immunisation is a distinct advantage;
- Demonstrated ability to motivate people of diverse background to resolving problems while promoting effective team work.

Duration of Support:
The duration of work for a consultant will be 3-4 months from signing of contract with monthly report submitted to IVD Team leader.

Fees and payment schedule:
The consultant will be paid as per NOC scale per month and allowances for travel will be provided including transport.

APPLICATION PROCEDURE
- The interested candidates should address an application comprising of a detailed Curriculum Vitae, Application letter, copies of certificates/diplomas/degrees and testimonials via the following link: **https://careers.who.int/careersection/ex/jobdetail.ftl?job=2202262&tz=GMT%2B03%3A00&tzname=Africa%2FNairobi**
- Deadline for submission of applications is Friday, 30th March 2022
- Qualified Females and disabled peoples are highly encouraged to apply.

N.B. Only shortlisted candidates will be contacted.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tumuenzi Hayati Magufuli kwa kuendeleza matamanio mazuri

NI mwaka mmoja sasa tangu aliyekuwa Rais wa awamu ya tano Tanzania, Dk. John Magufuli, kufariki huku ikiwa ni mara ya kwanza kwa nchi kukumbwa na msiba wa mkuu wa nchi akiwa madarakani, na kulazimu utaratibu wa kikatiba kufuatwa kwa aliyekuwa makamu wake kuwa Rais.

Rais Magufuli aliacha alama kwenye sekta ya miundombinu kuanzia ya barabara, usafiri wa majini na anga kwa kuhakikisha anafungua na kuunganisha maeneo yote ya usafiri ili watu, bidhaa na mazao wafanye majukumu yao bila kikwazo.

Pia, alihakikisha Tanzania inabaki na alama ya kuwa na Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo litazalisha umeme zaidi ya Megawati 2,115 na kuifanya nchi kujitosheleza kwa umeme, hata kuuza nje ya nchi na kujipatia fedha. Kwa sasa tuna daraja la Selander ambalo limeanza kutumika mwaka huu, limesaidia kupunguza foleni ya kuingia katikati ya Jiji la Dar es Salaam, pia kuna daraja la Busisi, mkoani Mwanza ambalo ujenzi wake unaendelea litakalowezesha wananchi kusafiri kwa barabara kwa haraka badala ya kutegemea Ziwa Victoria.

Barabara kuu nyingi zilijengwa na kwenye mitaa mbalimbali, mfano Dar es Salaam imekamilisha na nyingine zinaendelea kujengwa kwenye mitaa, jambo litakalorahisisha usafiri kwa wananchi na kupunguza foleni kwenye barabara kuu. Pia, alihakikisha ujenzi wa 'interchange' kwenye eneo la Ubungo, Tazara na Chang'ombe unakamilika ikiwa ni mkakati wa kupunguza foleni ndani ya jiji, lakini kuhakikisha watu hawapotezi muda mwingi kwenye usafiri.

Alama nyingine ni kufufua Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), na sasa lina ndege zinazofanya safari ndani na nje ya nchi, kuendelea kuitangaza Tanzania duniani, pia kununua ndege kwa fedha zetu bila mkopo, lakini kuwa na uhakika wa usafiri wa anga kwa kutumia usafiri wetu.

Matamanio ya Rais Magufuli ambaye alitokea kwenye Wizara ya Miundombinu ambayo aliimudu kiasi cha Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, kumuacha kwa miaka 10 kwenye wizara hiyo, aliyaendeleza kwa nguvu alipokuwa Rais hadi kuanzisha Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA), ili kuhakikisha zinajengwa kuwawezesha wakulima kusafirisha mazao na bidhaa nyingine kuyafikia masoko ya ndani na nje ya nchi.

Katika miradi hiyo ipo ambayo imekamilika, hatua mbalimbali na mingine kwenye mipango, yote inapaswa kukamilika, ili kuendelea kuweka alama, inapaswa kuendelezwa ili matamanio yake yatimie.

Alikuwa kiongozi mwenye uthubutu bila kujali lolote, aliwajengea imani Watanzania kuwa licha ya kuwa nchi yenye uchumi wa chini baadaye uchumi wa kati, wanaweza kuwa taifa kubwa kutokana na rasilimali Tanzania iliyojaliwa na kutembea kifua mbele kama nchi ya kutoa misaada.


Moja ya matukio ya uthubutu ni alipoamua kubadili matumizi ya Sherehe za Uhuru na kuzielekeza kwenye upanuzi wa barabara ya Morocco hadi Mwenge, ambayo ilikuwa na foleni kubwa nyakati za asubuhi na jioni, na sasa kuna barabara nne mbili za kwenda mjini na mbili za kwenda Mwenge. Mwaka mmoja wa Magufuli, tunawajibu wa kuendeleza mema yote aliyoyaanzisha kwa ajili ya Tanzania, kwa kuwa tunapokuwa na miundombinu tutayafikia masoko ya bidhaa na kwa urahisi, watu watasafiri kwa haraka kutoka eneo moja kwenda jingine.

Kila Rais hujitahidi anapokuwa madarakani miaka mitano ya kwanza ni kujenga nchi, mitano ya mwisho ni kuacha alama, lakini marehemu Magufuli alijitahidi kuacha alama kubwa kwenye miundombinu tangu alivyoingia madarakani, hakusita kuchukua hatua kwa haraka inapotokea mtu ameharibu.

Lazima Watanzania tulinde kwa wivu mkubwa kwa kuwa hakuna ubishi kuwa ujenzi wa miundombinu unatumia fedha nyingi, na wataalam wanatueleza kuwa kilomita moja ya barabara inagharimu Shilingi bilioni moja, hivyo unapoona zimejengwa kilomita kadhaa zote ni mabilioni ya fedha ambazo ni mkopo au fedha za ndani.

Mikopo inayochukuliwa italipwa na Watanzania wote hata ambao hawajazaliwa kwa kuwa inakopwa kwa ajili ya kufanya maendeleo, ndiyo maana tunasema kama namna ya kumuenzi Magufuli tulinde miundombinu hiyo ili idumu kwa miaka mingi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Yanayojadiliwa mkutano wa Hali ya Wanawake yafanyiwe kazi

Na Jenifer Gilla

KIKAO cha 66 cha Kamisheni ya Umoja wa Mataifa kuhusu Hali ya Wanawake (CSW66) kimeanza mkutano wake wa wiki mbili Machi 14, mwaka huu, ajenda kuu ni 'kufikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na wasichana wote katika muktadha wa mabadiliko ya hali ya hewa, sera na programu za kupunguza hatari za mazingira na majanga."

Dhima kuu ya mkutano huo mwaka huu, ni kuhakikisha wanawake wanapata nafasi sawa ya kushiriki katika ngazi za uamuzi katika mapambano dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi duniani.

Akiongea katika mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kutetea haki za Wanawake Duniani (UNWomen), Sima Bahous, anasema mkutano unaweza kutoa matokeo ya uthabiti na ufufuo wa ulimwengu ikiwa itaongozwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu ikiwamo kuungwa mkono na usawa wa kijinsia na kujitolea kwa pande nyingi, diplomasia, amani na haki.

Ili kupata matokeo chanya katika vita hivyo vya athari za mabadiliko ya tabianchi, ni lazima kuwapo michango ya jinsia zote kwa usawa, hivyo hatuna budi kufuta dhana na mfumo dume kuwa maamuzi makubwa yanafanywa na wanaume pekee na kuhakikisha kuwa ushiriki wa wanawake katika mapambano hayo unakuwa sawia na wanaume.

Wanawake wana mawazo muhimu sana katika janga hilo, kwa kuwa wana mchango mkubwa katika uwapo wake, hasa ukataji miti kwa ajili ya uhitaji wa nishati za kupika, suala ambalo udhibiti wake umekuwa mtihani, kwa sababu gharama zake ni nafuu kuliko nishati nyinginezo.

> **Ukiacha hivyo, kundi hilo ndilo waathirika wakuu wa matokeo ya tabia nchi kama kutumia muda mwingi kusaka maji, pale ukame unapozidi hali inayowasababisha kutoshiriki ipasavyo katika shughuli za maendeleo.**

Ukiacha hivyo, kundi hilo ndilo waathirika wakuu wa matokeo ya tabia nchi kama kutumia muda mwingi kusaka maji, pale ukame unapozidi hali inayowasababisha kutoshiriki ipasavyo katika shughuli za maendeleo.

Ukiacha kuchomwa na jua na kumaliza nguvu kazi wakisaka maji, pia wanaitia unyanyasaji wa kijinsia na kingono ikiwamo kubwakwa wakiwa njiani na hata kuambulia vipigo kwa wenzi wao kwa kuchelewa kurudi nyumbani na kufanya shughuli nyingine.

Hivyo basi, kama waswahili wasemavyo, 'siri ya kata aijuaye mtungi', ushiriki wa wanawake katika vita hivyo utaleta matokeo chanya. Kwa kuwa uzoefu wao katika tabu wanazopitia, utatoa majibu sahihi maswali yanayohitajika katika mapambano hayo.

Katika mkutano huo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, amekumbushia kuwa, ili kushughulikia upotevu wa uharibifu wa ardhi na uchafuzi wa mazingira, ni muhimu kwa kujenga maisha ya utu kwa wote na sayari zenye afya, hivyo ushiriki kamili na sawa wa wanawake na uongozi ni muhimu.

Shukrani za pekee ziifikie serikali kupitia Ofisi ya Rais Muungano na Mazingira, kwa kuandaa sera mpya inayoruhusu ujumuishwaji wa wanawake kuamua yake ya kimazingira. Hiyo inaonyesha kuwa serikali yetu imeona umuhimu ushiriki wa kundi hilo katika vita hiyo.


Itapendeza zaidi kama ushiriki huo ukianzia ngazi ya chini, yaani utendaji hadi ngazi ya juu ya uamuzi, ili kuleta matokeo chanya kwa mazingira himilivu katika nchi yetu.

TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

# TANROADS

## KUMBUKUMBU YA MWAKA MMOJA YA KIFO CHA MHE. DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI RAIS WA AWAMU YA TANO WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA




Mtendaji Mkuu, Menejimenti na Wafanyakazi wa TANROADS tunaungana na **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kumbukumbu ya mwaka mmoja ya kifo cha **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021.

**TANROADS** tutaendelea kumuenzi daima, kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii, Maarifa, Kasi na Weledi hususan katika utekelezaji wa miradi ya Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Barabara, Madaraja na Viwanja vya ndege kwa Maendeleo ya Taifa letu.

**BWANA ALITOA, BWANA AMETWAA JINA LAKE LIHIMIDIWE. AMINA.**

TANROADS Makao Makuu
Ghorofa ya 3, 10 Barabara ya Shaaban Robert / Garden Avenue
S.L.P 11364 Dar Es Salaam Baruapepe:Tanroadshq@tanroads.go.tz

***MIUNDOMBINU BORA YA BARABARA, MADARAJA NA VIWANJA VYA NDEGE KWA MAENDELEO YA TAIFA*** www.tanroads.go.tz

216753602

# Waandishi wanawake watakiwa kuandika habari zenye manufaa

**Na Beatrice Shayo**

WAANDISHI wa habari wanawake wametakiwa kuhakikisha wanaandika habari kwa umakini na zenye tija kwa ajili ya kubadilisha mitazamo ya jamii na kuepuka kuandika taarifa ambazo hazina ukweli.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, wakati akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari yaliyofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Msaada kwa Vyombo vya Habari (IMS).

Alisema kumekuwa na taarifa nyingi za uongo kwenye mitandao ya kijamii kwa sasa na kwamba kupitia kalamu za waandishi zinaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kutoa habari sahihi na zenye tija.

"Kuna taarifa nyingi za uongo katika mitandao na wengi wanakuwa na hofu kwamba vyombo vya habari vinaweza kukujenga asubuhi na kukubomoa jioni. Mwanamke wa Tanzania mmoja wa wale wamekuwa wahanga wa kubomolewa na vyombo vya habari na ni sehemu ya kujengwa na vyombo vya habari," alifafanua.

Waandishi mahiri, alisema ni wale waliopata taarifa zenye chanzo cha habari na kukiwa na uhakika nacho, unaanza kuifanyia kazi na si kuandika habari ya uongo.

Dk. Reuben alisema kutokana na mila na desturi za kitanzania, wanawake wa Tanzania na Afrika kwa ujumla, hawako tayari kuzungumza na vyombo vya habari, hivyo waandishi wa habari wanatakiwa kujifunza namna ya kuwawezesha ili wazungumze.

Pia alisema ni vyema mafunzo hayo waliyopata kuyachukulia kwa uzito kwa kuwa yanawezesha waandishi wa habari kujifunza na kuwajengea uwezo wa kuandika habari zenye tija.

"Mafunzo haya yatawawezesha kuwapa uwezo wa kutengeneza majina yenu kama waandishi wa habari jambo ambalo ni ndoto kwa kila mmoja kuwa mwandishi mahiri ndani ya nchi na nje ya nchi," alisema Reuben. "Imefika wakati taarifa nyingi za mitandaoni ambazo ni za uongo zinatakiwa sasa zijazwe na taarifa ambazo ni za ukweli na mwenye jukumu hilo ni wewe mwandishi kwani ni kazi yako kuandika taarifa zenye tija," aliongeza.

Mkurugenzi huyo alisema lengo la mradi huo ambao unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) kupitia IMS ni kuwasaidia wanahabari kuwa na uhuru wa kuzungumza na uhuru wa habari.

# Kunenge ataja sababu zinazochangia migogoro

**Na Julieth Mkreri, KIBAHA**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amesema vikwazo katika mkoa huo hususani migogoro ya wakulima na wafugaji vinachangiwa na baadhi ya viongozi na wananchi kutoheshimu sheria na taratibu zilizowekwa.

Kunenge aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua kongamano la viongozi wa dini lililofanyika mjini Kibaha kwa ajili ya kumuombea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, katika kipindi chake cha mwaka mmoja na kuombea nchi iepukane na majanga yakiwamo mauaji na unyanyasaji wa kijinsia.

Alisema hakuna sababu ya kuendelea kuwa na migogoro ya wakulima na wafugaji tatizo lililopo ni uadilifu ambao unachangia kuwapo na hali hiyo.

"Mkoa wa Pwani baadhi yetu hawaheshimu sheria baadhi ya vikwazo ni kutoheshimu sheria na taratibu tunapenda rushwa tunakiuka maadili yetu, tunajitahidi katika serikali yetu kuufungua Mkoa wa Pwani kupunguza maumivu," alisema.

Kunenge pia aliwaomba wazazi na walezi kuwasihi vijana wao kuacha tabia ya kuchagua kazi kwa madai ya kulipwa mishahara midogo jambo ambalo linasababisha kuendelea kuwapo mitaani bila kazi huku vijana kutoka nje ya mkoa huo wakichangamkia fursa.

"Hivi karibuni tunatarajia kufungua eneo kubwa kuliko yote Afrika la viwanda ambalo litaenda kuimarisha uchumi na kutoa fursa kwa wakazi wa Mkoa wa Pwani kushiriki katika mabadiliko ya kiuchumi," alisema. Kunenge alisema ni vyema viongozi wa dini, wazazi na walezi kuwaeleza vijana wao wasichague kazi wajitume na kufanya kwa bidii.

Alisema uamuzi uliofanywa na kamati ya amani kuandaa kongamano hilo kumuombea Rais katika mwaka mmoja wa uongozi wake ni jambo sahihi la kheri kwa taifa. "Uamuzi wa kongamano hili sio wetu kama serikali mmepanga wenyewe kama viongozi wa dini na kutukaribisha tunawapongeza kwa hili, sisi tuwaambie tumedhamiria kuufungua Mkoa wa Pwani tunachoomba ni msaada wenu katika maombi," alisema.

Alisema amani inatokana na haki na kukiwa na haki upendo na utulivu unakuwapo lakini pia bila kuwa na uchumi imara hapawezi kuwa na utulivu wala amani, viongozi wa dini pia wanatakiwa kukemea yale wanayoona yana upotoshaji.

Mwenyekiti mwenza wa kamati ya amani Mkoa wa Pwani, Hamis Mtupa, alisema kongamano hilo linalenga kumuombea Rais, kuiombea nchi iepukane na majanga, kupinga mauaji na unyanyasaji wa kijinsia na kutoa hamasa kwa ajili ya chanjo ya UVIKO-19 na ushiriki wa sensa.

"Kamati ya amani imejipanga kupiga vita, mauaji ndani ya Mkoa wa Pwani tumepanga kupinga jambo hili kwenye nyumba zetu za ibada na maombi yetu ya leo yatakuwa endelevu kwenye maeneo yetu," alisema. Mtupa alisema kamati za amani zikishirikishwa zinaweza kusuluhisha migogoro ya wakulima na wafugaji.

"Kamati za amani zikishirikishwa kuanzia ngazi ya juu hata kwa maombi zinaweza kuleta suluhu migogoro kwenye jamii na kwamba ipo ambayo kamati hiyo imefanikiwa kusuluhisha katika mkoa huo," alisema.

Mwenyekiti mwenza, Padri Beno Kikudo, alisisitiza kuwa suala la sensa si la serikali pekee, lakini pia hata kwenye vitabu vya dini limetajwa kuwa Yesu alishiriki kuhesabiwa na wananchi wanatakiwa kushiriki muda utakapofika.

Kongamano hilo liliwashirikisha viongozi kutoka katika dini ya Kikristo na Kiislamu, wazee mashuhuri na wakuu wa Wilaya wa Mkoa wa Pwani.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**
**MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA**

TMDA Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

## TANGAZO KWA UMMA

**16 Machi, 2022**

## KUANZA KUTUMIKA KWA KANUNI MPYA ZA ADA NA TOZO ZA MWAKA 2021

1. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) inapenda kuwajulisha wateja na wadau wote kuwa Kanuni mpya za Ada na Tozo za mwaka 2021 zimeidhinishwa na kutangazwa kupitia gazeti la Serikali, Na. 686 la tarehe 24 Septemba, 2021 kwa ajili ya utekelezaji.

2. Kufuatia hatua hiyo na kwa tangazo hili, viwango vipya vya Ada na Tozo kwa huduma zitolewazo na TMDA vitaanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 01 Aprili, 2022 kwa mujibu wa Kanuni za Ada na Tozo za Mwaka 2021 na si vinginevyo.

3. Aidha, malipo yote ya huduma yataendelea kufanyika katika akaunti za Benki za Mamlaka kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa malipo ya Serikali (GePG) baada ya kupata ankara kifani (profoma invoice) kutoka TMDA inayoonyesha namba maalum ya malipo (Control Number).

4. Wateja na wadau wote mnaombwa kuzingatia matakwa ya Kanuni hizi za Ada na Tozo za mwaka 2021 zinazopatikana kupitia tovuti ya TMDA ijulikanayo kama www.tmda.go.tz na/au ofisi za Mamlaka zilizopo Dar es salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Dodoma, Mtwara, Tabora pamoja na Geita kwa ajili ya utekelezaji.

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)**
**S. L. P 1253, Dodoma au S. L. P 77150, Dar Es Salaam**
**Simu: +255 222450512/ 2450751/ 2452108**
**Simu bila Malipo: 0800110084**
**Barua pepe: info@tmda.go.tz**
**Tovuti: www.tmda.go.tz**

216753902

# Shirika labaini kasoro miradi ya maendeleo

**NA Francis Godwin,** IRINGA

SHIRIKA la Maendeleo ya Jamii na Misitu Kanda ya Kitapilimwa (MJUMIKK), kupitia mradi wa ufuatiaji na uhajibikaji wa jamii (SAM) Wilaya ya Iringa limebaini kasoro katika utekelezaji wa miradi ya serikali na wadau.

Akizungumza jana wakati wa mkutano wa mrejesho wa shughuli za kamati ya SAM wilayani Iringa, Katibu Mkuu wa MJUMIKK, Mashaka Kilanga, alisema baadhi ya vijiji vya kata za Ilolompya, Mlenge, Masaka na Kiwere vina miradi mbalimbali ya kilimo inayotekelezwa hususani umwagiliaji, maghala na mashine za kukoboa mpunga.

Alisema katika ufuatiliaji kamati imebaini mambo kadhaa ambayo yanaweza kupunguza ufanisi au tija kwa wakulima ili kutokemeza umaskini na njaa.

Kilanga alisema miongoni mwa mambo hayo ni kama vile ukosefu wa mashine ya kukoboa mpunga katika ghala la Mlenge hali inayosababisha wakulima kuongeza gharama za usafirishaji mazao yao kupeleka sehemu zilizo na maghala na mashine za kukoboa.

Pia alisema kukosekana kwa miundombinu rafiki ya kuanikia mpunga pia unakwamisha ufanisi rafiki kwa ghala la Mlenge na pia ukosefu wa ushirika madhubuti unaweza kupunguza tija kwa wakulima kuongeza ufanisi wa ghala.

Kamati ya SAM Wilaya ya Iringa imejikita katika kufuatilia ufanisi wa miradi tajwa kwa lengo la kuongeza tija kwa wananchi, ambalo ni lengo kuu la serikali kukuza uchumi wa wakulima katika maeneo yao.

Diwani wa Ilolompya katika Tarafa ya Pawaga, Fundi Mihayo, aliupongeza mradi wa SAM kwa ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa katika maeneo yao, lakini akatoa angalizo kwa kamati hiyo kushirikisha wadau muhimu wakati wa ufuatiliaji.

Alisema kabla SAM haijawasilisha taarifa hiyo kwenye mkutano wa mrejesho, ijitahidi kuwaona watu wanahusika ili kuzifanya taarifa hizo kuwa bora zaidi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Dorah Mlomo, alisema mradi wa SAM katika masuala ya umwagiliaji na uboreshaji wa mazingira unasaidia katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Alisema kuwa wananchi wamekuwa na shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo zinatakiwa kufuatiliwa ili shughuli zao zisiharibu mazingira.

# Gwajima: Tanzania inatambua ushiriki wanawake kuleta matokeo chanya

**Na Mwandishi Wetu,** NEW YORK

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema Tanzania inatambua umuhimu wa ushiriki wa wanawake kuanzia ngazi ya chini katika jamii ili kuleta matokeo chanya.

Hatua hiyo, amesema itawezesha kutoa majibu na tija kwa changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa, mazingira na majanga kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.

Dk. Gwajima aliyasema hayo juzi jijini hapo katika mkutano wa mawaziri ndani ya Mkutano wa 66 wa Hali ya Wanawake Duniani.

Alisisitiza kuwa Tanzania inashiriki kikamilifu kwenye juhudi za kutunza mazingira, kudhibiti mabadiliko ya hali ya hewa na majanga. Kutokana na hali hiyo, alisema Tanzania imetia saini makubaliano mbalimbali yakiwamo Azimio la Beijing, Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Hali ya Hewa (UNFCC), Azimio la Kyoto 1997, Ajenda 2030 na CEDAW.

Katika hatua nyingine, Dk. Gwajima alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia kuwa kinara wa utekelezaji wa jukwaa la kizazi chenye usawa kwenye eneo la uwezeshaji wa haki za kiuchumi, eneo linalolenga kuwezesha uhakika wa upatikanaji wa chakula, uchumi na maisha bora kwa ujumla.

Aliongeza kuwa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa pamoja zinatekeleza Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia na kwa pamoja zimeandaa Sera ya Taifa ya Mazingira inayotekelezwa kwa ushirikiano na wadau ili kuwezesha jamii zilizo kwenye athari zaidi. Waziri Gwajima alisema Tanzania itafanya Sensa ya Watu na Makazi Agosti, mwaka huu, ambayo shabaha yake ni kutoa picha ya wakati wa sasa kuhusu hali ya hewa na mazingira kwa ujumla wake.

Amesema baada ya kutolewa taarifa hiyo, itasaidia wadau mbalimbali kushirikiana na Tanzania katika kufikia malengo ya kudhibiti athari za mabadiliko ya hali ya hewa na mazingira kwa kutengeneza sera, mipango na mikakati mizuri zaidi.

Dk. Gwajima ameongoza ujumbe wa Tanzania jijini New York kushiriki mkutano wa 66 wa Hali ya Wanawake Duniani uliojumuisha Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju.

Mkutano wa 66 wa Hali ya Wanawake Duniani ulianza Machi 14 na utaendelea hadi Machi 24. Pamoja na mambo mengine, utaangalia usawa wa jinsia katika sera, mipango na mikakati ya kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa, mazingira na majanga mbalimbali.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akiwasilisha taarifa ya nchi katika mkutano wa mawaziri ndani ya mkutano wa 66 wa hali ya wanawake duniani, jijini New York, nchini Marekani. Kushoto ni Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jinsia, Mwajuma Magwiza. **PICHA: WMJJWM**

# TAWA yaagizwa kuchimba visima katika vijiji vinavyozunguka mapori

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MWENYEKITI wa Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Meja Jenerali (mstaafu) Hamisi Semfuko, ameagiza kuchimbwa visima kwenye mapori 21 ya akiba.

Pia ameagiza kuchimbwa visima vya maji kwenye vijiji vinavyozunguka mapori hayo, ili kuondoa adha ya ukosefu wa huduma hiyo kwa wanavijiji ikiwa njia ya kudhibiti wananchi hao kutoingia kwenye mapori kufuata maji.

Jenerali Semfuko juzi kuwa kati ya Sh. bilioni 12.9 zilizotengwa kutokana na fedha za miradi ya maendeleo ya UVIKO- 19, kuna kiasi kilichotengwa kwa ajili ya ununuzi wa mashine (gari) na uchimbaji visima kwenye mapori ya akiba. Kutokana na mpango huo, alisema itapendeza kama zikitumika pia kuchimba visima kwa vijiji jirani.

Alisema mapori ya akiba yamekuwa yakikumbwa na ukosefu wa maji na kwamba kupitia fedha hizo, yatapata visima vya kutosha na kuondoa usumbufu wa wanavijiji kufuata maji kwenye mapori ya akiba.

Mwenyekiti huyo alisema itapendeza kama wananchi hao wakachimbiwa kisima kila kijiji na kwa kufanya hivyo watakuwa na imani na kuendelea kulinda mapori.

"Mtakapochimba visima kwenye mapori yetu, mkumbuke kuchimba na kwenye vijiji vinavyozunguka mapori ili kuwasaidia na wao kupata maji sambamba na kukuza ujirani mwema na kuboresha agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kumtua mama ndoo kichwani," alisema.

Pia alisema fedha hizo zimewasaidia kuinuka katika mambo mbalimbali ambayo walikwama kufanyika hasa kipindi cha mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 kutokana na kushuka kwa mapato. Alisema kabla ya ugonjwa huo mwaka 2016, mapato yalikuwa Sh. milioni 350 na mpaka bajeti ya mwisho mwaka 2019/20 yalipanda hadi kufikia Sh. bilioni 45 na walitarajia kupanda hadi kufikia Sh. bilioni 100 jambo ambalo halikuwezekana.

Kutokana na makusanyo ya mapato hayo ya utalii, mwaka 2016/17 walinunua magari 77 kwa mpigo ambayo yanaendelea kusaidia katika shughuli za usimamizi wa wanyamapori, uhifadhi na utalii kwenye mapori.

Naye Ofisa Mhifadhi Mkuu wa TAWA, Gisela Kimario, alisema kupitia fedha hizo, mamlaka inatekeleza miradi 32 ya miundombinu ambayo itagharimu Sh. bilioni 9.2.

Awali, Naibu Kamishna wa Uhifadhi wa Huduma za Shirika wa TAWA, Prosper Kyissima, alisema mamlaka imejipanga kuhakikisha miradi yote inayofanyika kukamilika kwa wakati na ubora unaokusudiwa.

# Asilimia 60 wahitimu Chuo CBE wanajiajiri

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimesema asilimia 60 ya wahitimu wake wanajiajiri na kuajiri wengine na kimeamua kujikita kwenye mafunzo ya vitendo ili kutatua tatizo la ajira.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Makamu Mkuu wa chuo hicho, (Taaluma, Utafiti na Ushauri), Profesa Edda Lwoga, wakati wa mkutano na Mameneja Rasilimali Watu (HRO) na masoko kutoka kampuni mbalimbali.

Alisema mkutano huo unalenga kupata mrejesho wa utendaji kazi wa vijana wanaohitimu kwenye chuo hicho na kujiweka sawa ili kutoa elimu inayoendana na elimu ya biashara kwenye soko la ajira.

Alisema mwaka 2016 chuo hicho kilifanya utafiti na kubaini kuwa asilimia 60 ya wahitimu wake wamekuwa wakijiajiri na kuajiri wenzao na ndiyo sababu wakaamua kujikita kwenye mafunzo ya vitendo.

"Tulifanya utafiti kwa kuwafuatilia wahitimu waliomaliza kwenye chuo chetu na kubaini kwamba asilimia 60 wamejiajiri na kuajiri wenzao na tulipata matokeo yaliyosababisha tufanye maboresho kwenye mitaala yetu," alisema.

Alisema kwa sasa wamekuja na mafunzo ya vitendo na mwanafunzi kwenye programu yake anakuwa darasani kwa nusu ya muda wake na muda mwingine anakuwa kwa mwajiri. Alisema wameamua kufanya hivyo ili kunoa ujuzi wa mwanafunzi ili hatimaye aweze kuajiriwa au kujiajiri mwenyewe anapomaliza masomo badala ya kuhangaika kutafuta ajira ambazo ni chache sana.

"Pia, tumeanzisha utaratibu ambapo mwanafunzi mwenye wazo la biashara anakuja nalo tunamtafutia mwalimu wa kumfundisha ili aweze kuanzisha kampuni yake na kufanya biashara na kuajiri wengine anapomaliza masomo yake hapa," alisema.

Naibu Mkuu wa chuo hicho, (Mipango na Fedha), Dk. Emmanuel Munishi, alisema kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya elimu ya biashara, chuo kimepanga kujipanua kwenda Zanzibar, Lindi na Iringa.

"Tumewaita nyie kwa sababu ndiyo mnaamua watu wafanye kazi kwenu au la kwa sababu nyinyi ndiyo mnahusika na kuajiri sisi kazi yetu ni kufundisha, nyinyi ni wadau muhimu sana kwa kuwa mnatengeneza mipango ya kuajiri," alisema.

"Tumewaita muangalie namna tunavyowaandaa hawa wafanyakazi wenu watarajiwa na sehemu ambazo tunatumia kuwaandaa mtshauri namna bora ya kuendelea mbele, tunataka mtshauri kwa sababu inawezekana bado tuna mtazamo wa zamani tuambieni tuendeje," alisema.

Alisema programu za CBE zimebadilika sana na wamefanikiwa kufanya maboresho makubwa kwenye miaka ya karibuni kutokana na mahitaji ya soko kubadilika.

Alisema chuo hicho kimeanzisha programu zaidi ya 26 na kwamba miaka minne iliyopita walianza kufundisha shahada mbili za Uzamili, lakini mpaka mwaka huu zimefikia 10.

"Tunatoa kozi za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) na Masoko kwa ajili ya kuleta wataalamu wenu kuja kuongeza elimu tumefundisha wataalamu wetu na sasa walimu 32 wamesoma mpaka kiwango cha PhD," alisema




Naibu Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), anayeshughulikia Mipango na Biashara, Dk. Emmanuel Munishi, akizungumza kwenye mkutano baina ya chuo hicho na maofisa rasilimali watu na masoko wa kampuni mbalimbali, chuoni hapo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# SHIVYAWATA yashukuru serikali kwa kujenga miundombinu rafiki madarasa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHIRIKISHO la vyama vya watu wenye ulemavu Tanzania mkoani Shinyanga (SHIVYAWATA), limeipongeza serikali kujenga vyumba vya madarasa kwa kuzingatia miundombinu rafiki ya watu wenye ulemavu.

Mwenyekiti wa SHIVYAWATA mkoani Shinyanga, Richard Mpongo, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake.

Alisema zamani ujenzi wa vyumba vya madarasa ulikuwa hauzingatii miundombinu rafiki ya watu wenye ulemavu, lakini sasa hali imebadilika na kuanza kujengwa na kuipongeza serikali katika ujenzi huo wa vyumba vya madarasa zitokanazo na fedha za UVIKO-19 kwa shule za sekondari na shikizi kuzingatia miundombinu hiyo.

"SHIVYAWATA mkoani Shinyanga, tunaishukuru serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, katika ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa shule za sekondari na shikizi, kuzingatia miundombinu rafiki ya watu wenye ulemavu," alisema Mpongo.

Pia, alitoa wito kwa taasisi zote za serikali, mashirika binafsi na madhehebu ya dini, wanapokuwa wanajenga majengo yao wazingatie miundombinu rafiki ya watu wenye ulemavu.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi binafsi ya Brother's, iliyopo kitangili Manispaa ya Shinyanga, ambao wanafundisha watoto wenye mtindio wa ubongo, alisema na wao katika shule yao wamezingatia miundombinu rafiki ya watu wenye ulemavu na kufanyia marekebisho madarasa ambayo yalikuwa hayana miundombinu hiyo.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema walipokea fedha za mapambano ya UVIKO-19, Sh. bilioni 17.4 kwa ajili ya maendeleo na Sh. bilioni 9.1 zilitumika kujenga vyumba vya madarasa 453, sekondari vyumba 393, shikizi 60, na vyote imezingatiwa miundombinu rafiki ya watu wenye ulemavu.

Rais Samia Suluhu Hassan alipokea fedha za mkopo Sh. trilion 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya mapambano ya UVIKO-19, na kuzielekeza kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa nchi nzima, ili wanafunzi wasisome kwa msongamano.

# Mila potofu kikwazo maendeleo ya wanawake

**Na Rose Jacob,** BUNDA

MILA potofu na desturi kandamizi bado ni tatizo kwa wanawake waishio vijijini wilayani Bunda, mkoani Mara kwa kushindwa kufanya mambo ya maendeleo kutokana na kukosa kipato.

Akizungumza katika semina ya wajasiriamali, Mratibu wa Miradi wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Dk. Bonamax Mbasa, alisema wameamua kujikita katika maeneo hayo na zaidi ya wanawake 700 waishio vijijini wilayani Bunda walipata mafunzo ya ujasiriamali.

"Wanawake wengi waliopo vijijini wamekosa matumaini ya kukua kiuchumi kupitia ujasiriamali, chanzo ni mila kandamizi, kukosa wazo la kibiashara, kutokuwa na taarifa muhimu zilizomo katika mpango wa biashara, kutokana na kukosa elimu ya sekta hiyo na watu wengi wamekuwa wakiandika mpango kazi kwa gharama kubwa," alisema Dk. Mbasa.

Alisema mafunzo waliyowapatia, ikiwamo kabla ya kuanzisha au kuboresha biashara zao, wanahitaji kukusanya taarifa muhimu na kufanya mipango inayo weza kuona iwapo biashara mpya itakuwa na manufaa ya kuchukua dhamana.

Akizungumza katika mafunzo hayo kwa niaba ya wanawake hao, mshiriki wa warsha hiyo, Rose Onesimo, alikishukuru Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini pamoja na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), kwa kutambua umuhimu wa wanawake wajasiriamali waliopo vijijini.

"Sisi wanawake tuishio vijijini kiukweli huwa tunajiona hatuwezi kufanya ujasiriamali ambao utatunyanyua kiuchumi na kimaendeleo, tumekuwa tukiwaona wenzetu walioko mjini wao ndiyo wanaweza, sasa tumeuona mwanga mzuri kupitia kwa watu wa Chuo cha Mipango na UNDP hivyo ni dhahiri tunakwenda kuondokana na umaskini wa kipato," alisema Onesmo.

Vile vile, alisema hapo awali biashara zao zimekuwa haziendelei kutokana na kufanya ilimradi na mtaji huo ndiyo unakuwa wa kujikimu kimaisha na familia, mila potofu ni tatizo kwao, wanaume wanaona mwanamke akiwa na kipato na yeye sichochote. Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Charles Malunde alisema, wanawake walioko vijijini wanapaswa kutambua ujasiriamali siyo biashara pekee ya bidhaa zingine hata kilimo na ufugaji ni ujasiriamali unaoleta tija katika familia.

"Kumekuwapo na tabia ya watu kuwapatia mafunzo wanajamii, lakini wameshindwa kuja na utatuzi leo (jana) tumeona wenzetu wa Chuo cha Mipango na UNDP wameleta warsha hii vijijini na wametafuta benki ya CRDB kwa ajili ya kuwapatia mikopo ya mitaji walengwa hao, hii inaleta maana kubwa ya kuonyesha tija kwa wananchi kupata ufumbuzi," alisema Malunde.

ama

ALHAMISI MACHI 17, 2022

AFYA NA MAZINGIRA





Ukurasa 13

MSD rasmi katika uzalishaji dawa, Makambako sehemu ya wanufaika



Ukurasa 14

Kipaumbele kutathmini mlipuko wa Uviko, kisha kwenye chanjo rasmi

MWAKA MMOJA KIFO CHA JPM

# Umma 'unavyomisi' burudani zake hulka, mbwembwe, hata upendo

**Na Sabato Kasika**

LEO ni mwaka mmoja umetimia tangu Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli afariki dunia, Machi 17 mwaka jana na kuacha taifa katika simanzi kubwa. Ni uzoefu wa mara ya kwanza kwa Watanzania kushuhudia kifo cha Rais akiwa madarakani.

Mara baada ya kuingia madarakani mwaka 2015, aliibuka na kaulimbiu ya 'Hapa kazi tu' iliyolenga kuhamamisha Watanzania hasa vijana kujishughulisha kwa ajili ya kujiletea maendeleo badala ya kukaa vijiweni au kucheza mchezo wa 'pool'.

Rais Dk. Magufuli, pia alikuwa na hulka ya aina yake katika utendaji kazi ambao ulikuwa kivutio na kuwafanya watu wa kada mbalimbali kuwa karibu na vyombo vya habari wanaposikia yuko kwenye ziara mahali fulani, kila mmoja akidadisi 'nini kinatokea' kutokana na jinsi alivyokuwa akifanya maamuzi ya papo kwa hapo, ili asiwacheleweshee majibu Watanzania.

Hilo alilifanya ama kwa mazuri au aliyoyaona yana ukakasi. Hapo kuna ya kukumbukwa. Mathalan, hata katika kuidhinisha Manispaa ya Dodoma kuwa jiji, hakusubiri mchakato, bali ushuhuda wake na kuridhika na uhalisia akaufanya uamuzi mkutanoni.

Ndiyo aina ya uamuzi alioufanya hata kwa Halmashauri ya Kahama kuwa Manispaa. Pia , wakati fulani akiwa kwenye mkutano wa kisheria akawatangazia wanazuoni hao alivyokuwa na hukumu iliyoandikwa na Jaji wa Mahakama Kuu, hata akatangaza



Rais Dk. John Magufuli akionyesha umahiri wa 'kucheza tumba' katika muziki wa dansi, zama za uhai wake. **PICHA: MAKTABA**

kumpandisha hapo kwa hapo mkutanoni kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.

Vivyo hivyo, kwa yaliyomkera, akawa na uamuzi wa papo kwa hapo kwa watendaji waliotuhumiwa kwenda kinyume na utaratibu aliyaita kwa jina la 'kutumbua' au wakati mwingine alisikiliza malalamiko ya watu katika mikutano ya hadhara na kuyatolea maamuzi.

Huyo ndiye JPM anayetimiza mwaka mmoja tangu kufariki, mrithi wake Rais Samia Suluhu Hassan, naye akipita katika nyayo hizo, wote wakiwa katika historia ya kuwatumikia Watanzania kila mahali waliko.

Kwa wale ambao hawakubahatika kufuatilia hulka za JPM katika utendaji kazi, niwamegee kwa

INAENDELEA UK.12

# Umma 'unavyomisi' burudani zake hulka, mbwembwe, hata upendo



Namna alivyokuwa, Dk. John Magufuli, nyumbani kwao Chato akijumuika na jamii kwenye vijiwe. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

**INATOKA UK.11**

uchache ili kuwakumbusha wakati huu ambao anatimiza mwaka mmoja tangu alipotangulia mbele ya haki.

**NYENDO ZAKE**

Kupiga 'pushapu': Kwa wale wanaliokuwa wakifuatilia kampeni zake katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, watakuwa wanakumbuka jinsi alivyokuwa akipiga 'pushapu' jukwaani kabla ya kunadi sera za chama chake akiashiria kuwa yuko imara kuwatumikia Watanzania.

'Pushapu' hizo hazikuishia kwenye kampeni za uchaguzi mkuu tu, pia alikuwa akikumbushia hata kwenye mikutano ya hadhara katika ziara zake katika mikoa mbalimbali nchini.

Utamu wa mbwembwe zake kwa umma, ulikuwa ni pale katika ziara yake inapokuwapo bendi ya muziki wa dansi, akimaliza kuhutubia ni lazima ashuke jukwaani na kujichanganya na wanamuziki akipiga kifaa tumba au ngoma kwa umahiri wa kiuanamuziki .

Ziara za ghafla: Katika utendaji kazi wake alikuwa na kawaida ya kufanya ziara za kushtukiza katika maeneo ikiwamo Wizara ya Fedha, bandarini kwenye taasisi mbalimbali na Ofisi Ndogo ya CCM Makao Makuu katika Mtaa wa Lumumba, Dar es Salaam, hali iliyowafanya watendaji kutarajia mgeni wake wakati wowote kutoka kwenye ziara hizo za ghafla.

Wakati mwingine, aliweza kwenda ufukweni katika 'kijiwe' cha uvuvi feri, ambako ni jirani na Ikulu Dar es Salaam, akazungumza na wachuuzi wa samaki na kuna wakati, alitembea hadi penye huduma za kibenki 'ATM', hali iliyoleta burudani kwa kila mmoja, wengi wakimuona 'huyu ni Rais wa Watu.'

> **'Pushapu' hizo hazikuishia kwenye kampeni za uchaguzi mkuu tu, pia alikuwa akikumbushia hata kwenye mikutano ya hadhara katika ziara zake katika mikoa mbalimbali nchini.**



Sehemu ya hulka yake, Marehemu Dk. John Magufuli, akifurahisha umma kwa kuonyesha uwezo wake wa mazoezi ya 'push –up' kwenye mkusanyiko wa mkutano wake.

Nadharia ya kutumbua majipu: Wale waliofanya kazi kinyume na utaratibu, watakuwa wanamkumbuka jinsi alivyohakikisha kila mmoja anarudishwa mstarini kwa lazima na kutumika inavyotakiwa. Mtindo huo wa 'kutumbua majipu' ulijipatia umaarufu mkubwa kitaifa na kimataifa.

Umahiri wa lugha nyingi nchini: Inawezekana Rais Dk. Magufuli, alikuwa miongoni mwa Watanzania wachache waliojaliwa uwezo wa kuzungumza lugha za makabila mengi nchini.

Hiyo inatokana na kwamba alikuwa na kawaida ya kuzungumza lugha hizo ikiwamo kikurya, kichaga, kijita, kipare, kigogo, kihehe, kihaya, kiha, kinyakyusa na nyingine nyingi.

Mtindo wake wa kuzungumza lugha za makabila mbalimbali ulikuwa unamfanya avutie watu wengi na kumshangilia, huku wakati wote hakusahau masihara na watani wake.

Dk. Magufuli katika kampeni zake za kuwania kuwa mteule wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kwa bendera ya chama chake , aliibuka na mtindo tofauti wa kufanya kampeni ya uteuzi pasipo kushuhudia wapambe kama ilivyokuwa imezoeleka kisiasa, hata kuja wakati akiwa pekee na dereva wake.

Anapania haikachi: Kawaida yake ilikuwa kwamba, akipania kufanya mradi, 'piga ua; lazima ahakikishe unakamilika. Kwa mtindo huo, amefanikisha miradi mbalimbali, baadhi inashuhudiwa sasa imekamilika na mingine inaendelezwa na awamu iliyopo ya uongozi.

Mojawapo inabaki kuwa alama yake ni kuhamisha makao makuu ya nchi kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma, ambapo ujenzi wa Ikulu unaendelea.

Mdau vijiwe kahawa: Anapokuwa na nafasi na hasa nyumbani anapokuwa kwao Chato, daima aliibuka kwenye vijiwe vya kahawa kupata kinywji hicho na kuzungumza mawili, matatu na wauzaji pamoja na watu wengine wanaokuwapo kwenye vijiwe hivyo huku utani ukiwa mwingi zaidi.

Baadhi ya maeneo ya vijiwe vya kahawa ambavyo aliwahi kwenda ni katika soko la Feri jijini Dar es Salaam na nyumbani kwao Chato mkoani Geita ambako pia ilikuwa ni kawaida yake kukatisha mitaa ya mji wa Chato kusalimia wananchi ambao awali alikuwa mbunge wao, huku akielezea 'kuwamisi' tangu alipochaguliwa kuwa Rais.

JPM na lugha: Mojawapo ya vitu ambavyo alikuwa akishangaa, ni baadhi ya watu kudai kwamba hajui kuzungumza lugha ya Kiingereza na kuweka wazi kuwa huo ni uzushi ambao haukuwa na maana yoyote, huku akihoji alivyokuwa ughaibuni alikuwa anazungumza lugha gani.

Pia, hili liliendana sana na kuwa muumini wa Kiswahili, msisitizo wake ulikuwa kuimarisha lugha ya Kiswahili ili kutumika katika mahakama zote huku sheria zikiwa zimetafsiriwa kwa lugha hiyo ili iwe rahisi kwa Mtanzania wa kawaida kuzielewa.

Tayari alishaanza juhudi kutaka kutafsiriwa sheria kwa Kiswahili kama ambavyo alielekeza, lakini pia alitamani lugha hiyo iwe ya kufundishia kuanzia elimu ya msingi hadi chuo kikuu, huku akiwa na historia mikutano mikubwa kama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), uliofanyika nchini 'alishusha' hotuba kwa Kiswahili.

Itoshe kusema kuwa, 'alipangalo Mungu binadamu hawezi kulipangua', ameamua kuchukua kiumbe chake, hivyo nimalizie kwa kurudia kwamba 'tunazimisi' hulka hizo za JPM.

AFYA

# MSD rasmi katika uzalishaji dawa, Makambako sehemu ya wanufaika

**Na Mary Geofrey, aliyekuwa**

**Makambako**

BOHARI Kuu ya Dawa (MSD), kwa sasa inatekeleza miradi minne ya ujenzi wa viwanda vya dawa na vifaa tiba nchini, ili kupunguzia serikali mzigo wa kuagiza dawa nje ya nchi kila mwaka.

Kukamilika ujenzi huo kutasaidia kuokoa Sh.bilioni 33 kila mwaka na kupunguza mahitaji ya kuagiza dawa kutoka nje ya nchi, kutoka asilimia 90 za sasa hadi asilimia 75 na 60.

Mradi wa ujenzi wa viwanda hivyo ulianza rasmi Oktoba 4, mwaka juzi ukigharimu Sh. bilioni 16.7, ukilenga kuanzishwa Kiwanda cha Mipira ya Mikono (glovu).

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Bohari ya Dawa (MSD), Erick Mapunda, anayezungumza kwa Niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Meja Jenerali Gabriel Mhidze, anawaambia waandishi wa habari kwamba, kukamilika kwa ujenzi huo ndani ya miezi mitatu ijayo, kutasaidia uzalishaji jozi ya glovu 20,000 kwa saa.

Anasema, aina nyingine ya dawa itakayozalishwa ni vidonge vya rangimbili 330,000 zitakazozalishwa kwa saa na vidonge vya kawaida, ambavyo vitazalishwa 425,000 kwa saa moja.

"Dawa hizo ni Paracetamol, Amoxycillin, Arythromycin, Ampiclox ambazo zinahitajika kwa wingi nchini," anasema Mapunda na kufafanua zaidi kuwa kiwanda pia kitazalisha dawa za maji chupa 180 kwa saa za kuhudumia kikohozi, maumivu, cotrimoxazole syrup na metronidazole syrup.

"Ujenzi wa kiwanda hiki umekamilika kwa asilimia 90 na uzalishaji wa majaribio tayari umeshaanza na kuonyesha mafanikio makubwa," anafafanua Mapunda.

### KIWANDA CHA GLOVU

Mapunda anasema ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha mipira ya mikono ulianza rasmi Oktoba mwaka 2020, ukijumuisha jengo la kiwanda lenye ukubwa wa mita za mraba 3120.

Anaeleza kuwa, ujenzi wa kiwanda hicho umekamilika kwa asilimia 90 na uzalishaji wa majaribio umeshaanza na kuonyesha mafanikio makubwa.

Anasema, pia kuna ghala la kuhifadhi malighafi linaloendelea kujengwa lenye ukubwa wa mita za mraba 1,000. Ulianza Septemba mwaka jana na unatarajiwa kukamilika baadaye mwaka huu.

Mapunda sasa anasema, eneo linalozungushiwa uzio lina ukubwa wa ekari 38, uzio husika unajengwa kwa zege na matofali ya kuchoma, uzio una urefu wa mita 2.2 na urefu wenye jumla ya mzingo wa mita, 680 ambayo ni sawa mita za mraba 3,696.

"Mpaka sasa ujenzi wake umefikia asilimia 90 na unatarajiwa kukamilika katika robo ya tatu ya mwaka 2022," anasema.



Ndivyo ilivyo, kazi ikiendelea ya ujenzi wa miundombinu ya kiwanda cha dawa kilichoko Makambako kinachomilikiwa na MSD. **PICHA: MARY GEOFREY**



### MAJENGO YA VIWANDA

Ujenzi wa Majengo ya viwanda vya dawa za vidonge, dawa za maji na vidonge vya rangi mbili, unaohusisha ujenzi wa majengo matatu yanayofanana kwa ukubwa wenye mita za mraba 900.

Anasema mpaka sasa majengo yote matatu yamekamilika kwa asilimia 90 na yanatarajiwa kukamilika baadaye mwaka huu na kupokea mitambo ya kuzalisha dawa vimiminika, rangi mbili na dawa zingine.

"Hadi Desemba mwaka jana, ufungaji wa mifumo ya maji na mitambo pamoja na eneo la usafi unaendelea," anasema Mapunda.

Kwa sasa MSD imeshanunua mitambo ya kutengeneza na kufungasha dawa rojorojo ambayo imeshawasili nchini katika eneo la mradi, MSD makao makuu Keko na makpio yake yamefanyika kwa asilimia 60.

"Uzalishaji bidhaa za afya utaanza kwa kila kiwanda pindi ujenzi wake utakapokamilika," anaeleza Mapunda kwamba usimamizi wa mradi ujenzi wa viwanda unatekelezwa na kusimamiwa na MSD, ikishirikiana na makandarasi waliotengeneza mitambo ya viwanda hivyo kutoka China, MSD ina watumishi 14.

### AJIRA ZA WATANZANIA

Mradi unatajwa kutoa ajira za moja kwa moja kwa wakazi 196 Makambako, zikiwamo ajira zisizo za moja kwa moja kama Mamalishe, wachimba kokoto wachimba kifusi wapakiaji mchanga na kokoto na kampuni za usafirishaji vifaa na malighafi za ujenzi.

> "Pamoja na juhudi kubwa inazofanya Wizara ya Afya, ni pamoja na kujenga viwanda vya kuzalisha dawa na vifaa tiba nchini ili kuwekeza sekta ya viwanda, pia kuipunguzia mzigo serikali wa kuagiza dawa nje ya nchi.

Mapunda anaeleza zaidi kuwa, changamoto ni upatikanaji malighafi ya utomvu aina ya Latex, anasema juhudi za kutafuta malighafi hiyo maeneo ya Tanzania Bara zinaendelea.

"Jitihada zinaendelea kupatiwa mashamba ya miti (aina ya rubber) kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mazungumzo yanaendelea kwani upatikanaji wa malighafi hii ndani ya nchi utapunguza gharama za kuagiza kutoka nje ya nchi," anaeleza Mapunda.

Kingine katika sababu nyingine ni kuchelewa kufika wataalamu, kutokana na janga la UVIKO 19:"Baadhi ya wataalamu wa kufunga mitambo kutoka China walichelewa kuwasili nchini, hivyo kuathiri ukamilishaji wa ufungaji mitambo."

### KAZI ILIYOBAKI

Mhandisi Mradi huo, Shiwa Mushi, anaeleza zaidi kuwa kwa sasa ufungaji wa eneo la usafi, vyoo vya ndani ya kiwanda na maeneo ya kubadilishia nguo unaendelea.

"Ujenzi wa ghala hili ulianza rasmi Septemba 10, mwaka jana na unatarajiwa kukamilika katika robo ya tatu ya mwaka 2022,"anasema Mushi.

Kaimu Mkurugenzi Kitengo cha Mawasiliano, Wizara ya Afya, Catherine Sungura, anasema katika mafanikio ya serikali, hivi sasa kiwanda kiko katika mafanikio makubwa katika rekodi ya kiserikali.

"Pamoja na juhudi kubwa inazofanya Wizara ya Afya, ni pamoja na kujenga viwanda vya kuzalisha dawa na vifaa tiba nchini ili kuwekeza sekta ya viwanda, pia kuipunguzia mzigo serikali wa kuagiza dawa nje ya nchi," anasema Catherine.

### WENYEJI MAKAZI

Mwenyekiti wa Mtaa wa Idofi, Kata ya Mlowa, Junusi Muhelela, anaishukuru serikali kwa ujio wa kiwanda hicho kwa kujengwa kwenye mtaa huo, kwani umewasaidia vijana kupata ajira na kupunguza changamoto za uhalifu, ikiwamo wizi mitaani.

Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Idofi, Emanuel Hauli, anasema kiwanda hicho kimesaidia kuongeza thamani ya ardhi katika kijiji hicho. Anafafanua; "Zamani tulikuwa tunanunua ardhi kwa thamani ya chini lakini sasa tunaona thamani imepanda lakini pia tumepata wawekezaji mbalimbali wanaokuja kutaka kuwekeza hapa."

Anaiomba serikali kuwajengea hospitali mahali hapo, ili iwahudumie wananchi na wanufaike moja kwa moja na huduma za dawa na vifaa tiba vinavyozalishwa kijijini hapo.

AFYA

# Kipaumbele; katathmini mlipuko wa Uviko, kisha kwenye chanjo rasmi

## • Sasa huduma ipo kila zahanati

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA awamu ambayo Rais Samia Suluhu Hassan yupo madarakani kwa wadhifa wa sasa, kukashuhudiwa awamu nyingine ya msukosuko wa maradhi ya Uviko 19.

Pia, ni zama ambayo Rais Samia akafikia hatua ya kutaka Watanzania kuanza kuchanjwa, ilhali msingi wa uamuzi wa mtu kuchanja hadi sasa ni hiari.

Katikati ya mwaka jana, taifa lilipokea shehena za dawa aina ya Johnson&Johnson kutoka nchini Marekani, huku Rais Samia akizindua kampeni maalum, hatua iliyoendana na binafsi kushiriki chanjo, akiambatana na maofisa waandamizi wa kiserikali kwenye tendo hilo.

Kupokewa msaada wa dawa hizo, kuna sura ya pili kwa Tanzania katika diplomasia ya kimataifa, Rais Samia akiwa katika ishara ya kuendeleza mafanikio hayo ndani ya uongozi wake.

Ingawaje kuna mjadala mkali ambao umekuwa ukiendelea kuhusu uhalali wa chanjo, Rais Samia akatumia maelezo ya kina katika uamuzi wake huo wenye maslahi mapana kitaifa na kimataifa

"Mimi niko tayari kuchanja sasa hivi..." akatamka Rais Samia, muda mfupi kabla ya kuchoma chanjo,

Shirika la Afya Duniani (WHO), ndio lililoidhinisha chanjo hizo zinazotengenezwa kutoka nchi zilizoendelea. Pia likaweka miongozo yake na shehena ya kwanza ya Chanjo Johnson, zilikuwa zaidi ya milioni moja.

Wakati Rais Samia, akifafanua kuwa chanjo ni imani, pia akaipa jukumu iliyokuwa Wizara ay Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, jukumu la kuelimisha umma, umuhimu wa chanjo hiyo akitaja mikoa kadhaa hali haikuwa nzuri katika wimbi hilo la latu wakati huo.

Katika ufafanuzi wake, aliyekuwa Waziri wa Afya wakati huo, Dorothy Gwajima, ambaye kitaaluma ni daktari, akasema hashangai hoja na mitazamo hasi inayotolewa dhidi ya chanjo hizo, ila wao wizara husika wako tayari kujitolea kwa ufafanuzi.

Wakati huo inatangazwa, takwimu zilizotangazwa kitaifa ziligota katika wastani wa wagonjwa 100.


Hatua hizo za kupatikana chanjo hizo, ni zao la lililotamkwa na Rais Samia, kwamba tayari nchi imeshajiunga na Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Kuchagiza Upatikanaji wa Chanjo -COVAX kwa nchi za kipato cha chini.

Miongoni mwa nchi za Afrika ambako tayari COVAX imewasilisha chanjo zinatajwa ni pamoja na Rwanda, Uganda, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).



Siku Rais Samia Suluhu Hassan, alipochoma chanjo dhidi ya Corona. **PICHA: MTANDAO**

> **Pamoja na mapendekezo haya, Kamati Huru ya Kitaifa ya Ushauri wa Chanjo (NITAG) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ziendelee kushirikishwa katika kutoa ushauri na kudhibiti chanjo hizo.**




### MIZIGO YA DOZI

Serikali ya Marekani imeipatia Tanzania zaidi ya dozi milioni nne za chanjo dhidi ya UVIKO 19, ikianzia na wastani wa dozi milioni 1, Julai mwaka jana.

Pia, msaada wa zaidi ya dozi milioni 3.5 za chanjo aina ya Pfizer BioNTech zilizoletwa kwa awamu tatu kati ya Novemba mwaka jana na Januari mwaka huu. Tanzania imo katika orodha ya nchi lengwa katika Mpango wa Serikali ya Marekani wa Kupata Chanjo Duniani (Global VAX), unaolenga kuongeza chanjo za kukabili maradhi UVIKO-19.

### KUTOKA CHINA

Pia, hadi kufika Novemba hatua zaidi ya chanjo kukabili Uviko 19, ikiwa itikadi ya afya kimataifa kutoka kwa Rais Samia, juhudi za Tanzania zikaungwa mkono na China kwa kupewa dozi 500,000 dawa aina ya Sinopharm.

Aidha, Januari mwaka huu, awamu nyingine ya dozi 800, 000 kutoka China zilipokewa katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Katika halfa hiyo, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliyepokea mzigo huo kutoka kwa Balozi wa China, Chen Mingjian, ambaye aliahidi kwamba wakati kirusi kipya 'Omicron' kikivinjari duniani, nao Wachina wako imara katika hatua ya kuhakikisha wanatumia nguvu zote kukikabili kwa mafanikio .

Hadi sasa hatua iliyofikiwa katika usambazaji chanjo kukabili virusi vya Covid 19, ni kwamba serikali imewezesha kupatikana huduma katika ngazi zote zikiwamo zahanati za umma na binafsi nchini.

### UAMUZI ULIVYOFIKIWA

Mnamo Mei mwaka jana, akiwa na miezi kadhaa katika nafasi yake, Rais Samia alipokea ripoti ya kitaalamu kutoka kwa Profesa Said Aboud, ambayo ilimthibitishia ' Chanjo ya Corona ni salama na fanisi.'

Kamati maalum ya Corona Tanzania iliyoundwa na Rais Samia mwezi mmoja kabla, ikamthibitishia usalama huo pia kuonyesha ufanisi, hata kuishauri serikali kupitia vyombo vyake, kulishughulikia suala la chanjo kwa kujiunga na Mpango wa Covax, chini ya mwamvuli wa Gavi.

Mpango huo wa Covax unalenga kuhakikisha nchi masikini zote duniani zinapata mgao sawa wa chanjo, licha ya ufinyu wa uwezo wao kiuchumi.

Pia, mwamvuli wa Gavi unaundwa na mashirika mbalimbali ikiwamo WHO na baadhi ya serikali za nchi tajiri duniani.

"Kamati inashauri serikali kwa kutumia vyombo vyake iendelee na hatua kuelekea kuruhusu matumizi huru ya chanjo dhidi ya ugonjwa wa Covid -19, kwa kutumia chanjo zilizoorodheshwa na Shirika la Afya Duniani, ili kuwapa fursa ya kinga wananchi wake, kwa kuwa kupitia uchambuzi wa Kamati, chanjo hizo zina ufanisi na usalama unaokubalika kisayansi," akaeleza Profesa Aboud, kutoka Chuo Kikuu cha Afya cha Muhimbili na Mwenyekiti wa kamati hiyo.

"Pamoja na mapendekezo haya, Kamati Huru ya Kitaifa ya Ushauri wa Chanjo (NITAG) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ziendelee kushirikishwa katika kutoa ushauri na kudhibiti chanjo hizo," anaeleza mtaaluma na Mwenyekiti wa Kamati, Profesa Aboud.

Kamati hiyo ikapendekeza matumizi huru ya chanjo nchini Tanzania, ikimaanisha hakutakuwapo mtu atakayeshurutishwa kuchoma chanjo kinyume na matakwa yake binafsi.

Hata hivyo, kamati ikawa na pendekezo pale chanjo itakapoingia Tanzania, kuwapo makundi maalumu kadhaa ambayo yangepewa kipaumbele katika utoaji wa chanjo, kama vile wazee, lakini hatua iliyofikiwa sasa huduma hiyo inapatikana kila mahali na kuna utaratibu maalum kwa wanaosafiri nje ya nchi.





## Aomba wasanii wapewe elimu ya sensa kufikisha ujumbe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

IKIWA imesalia miezi mitano kufanyika kwa Sensa ya Watu na Makazi nchini, Mwimbaji wa nyimbo za injili, Rose Muhando, ameiomba serikali kutoa elimu kwa wasanii kuhusu umuhimu wa sensa ili kurahisisha kufikisha ujumbe kwa jamii.

Muhando, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya serikali ya awamu ya sita katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema sensa hiyo ni jambo la kitaifa na kila Mtanzania anatakiwa kushiriki kikamilifu ili nchi ipate takwimu sahihi kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

"Serikali itenge muda wa kuelimisha wasanii umuhimu wa sensa kwa kuwa sensa sio ya watu fulani hata Yesu alipozaliwa kwenye holi la ng'ombe alizaliwa katikati ya tukio la kuhesabiwa, hivyo lazima tujitokeze katika jambo hili la kitaifa."alisema

"Na kwa Mungu kutohesabiwa ni dhambi kama ilivyo kwenye kutopiga kura, huwezi kutambulika katika taifa lako kama hujahesabiwa hivyo wasanii wenzangu tujitokeze kushiriki katika zoezi hili kuhesabiwa pamoja na kuhamasisha watu wajitokeze," alisema Mhando.

Akizungumzia mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani, Muhando alipongeza kwa namna ameiongoza nchi katika kipindi hicho.

"Mama Samia amepambana sana katika kuhakikisha kuwa miradi yote ambayo iliachwa na mtangulizi wake Hayati Magufuli inakamilika kama ambavyo ilikuwa imepangwa awali," alisema Mhando.

Alisema pia katika kipindi cha mwaka mmoja Rais amejitahidi kuondoa matabaka yaliyokuwapo na kuwafanya Watanzania kuwa na umoja.

"Watanzania tumekuwa na umoja wa kitaifa, lakini pia Rais Samia ameweza kuiunganisha na mataifa mengine kuwa na ushirikiano na mataifa mengine duniani," alisema.

Alisema pia anampongeza Rais kwa kuwezesha wasanii kuanza kupata mirabaha kutokana na kazi ambazo wamekuwa wanazifanya kwenye tasnia hiyo.

"Mimi tangu nimeanza kazi hii ya kuimba sikuwahi kupata hata Sh. 30,000, lakini kwa mara ya kwanza katika utawala wa mama Samia nimepata zaidi ya Shilingi milioni tano kwa hili nampongeza sana inatujengea motisha wasanii katika kazi zetu mbalimbali nchini," alisema.

# Serikali yatangaza neema katika uwekezaji kilimo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imetangaza neema ya uwekezaji katika kilimo nchini ili kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo na kuongeza Pato la Taifa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Balozi Dk. Pindi Chana, alitoa kauli hiyo jana alipofanya mazungumzo na Mwakilishi wa Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa (WFP) Tanzania, Sarah Gibson na Mkurugenzi wa Shirika hilo Kanda ya Kusini mwa Afrika, Dk. Manghestab Haile, Ofisini kwake jijini hapa.

Alisema Tanzania ni sehemu salama kwa ajili ya kufanya uwekezaji katika nyanja ya kilimo, wawekezaji wanakaribishwa kuchangamkia fursa hiyo.

Pia, katika kikao hiko masuala yaliyoafikiwa ni kuboresha suala la lishe kwa wananchi kwa kuwa licha ya kuwapo uzalishaji mkubwa wa chakula katika maeneo mbalimbali bado kuna tatizo la utapiamlo.

"Tunaposhirikiana na WFP chini ya Rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan Tanzania ni eneo sahihi kabisa katika uzalishaji wa chakula tumekuwa tukizalisha chakula cha kutosha na tumekuwa mfano nchi yetu ya Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki na Nchi za SADC na tumekuwa tukipeleka chakula nje ya Nchi," alisema.

Waziri Pindi alisema pia wamekubaliana kushirikiana katika masuala ya maafa pindi yanapojitokeza kwa kuwa yamekuwa yakisababisha maafa kwa raia.

Alibainisha kuwa wamekubaliana kuboresha suala la kilimo kuendana na teknolojia iliyopo sasa na matumizi sahihi ya pembejeo sambamba na ushirikishwaji wa vijana katika uzalishaji wa chakula, masoko na kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo.

"Tumezungumzia suala la matumizi ya vitendea kazi vya kisasa, ushirikishwaji wa vijana maana idadi kubwa ya umri wa watu ni vijana na sasa tunaelekea katika sensa ya watu na makazi mwaka huu kwa hiyo ni jinsi gani tunahamasisha vijana katika uzalishaji wa chakula na kuongeza thamani yake," alieleza.Aliwahakikishia kuwa katika bajeti ijayo serikali imeweka nguvu kubwa kwenye sekta ya kilimo ili kuwa na tija.

Naye, Mwakilishi wa WFP, aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha taifa linakuwa na chakula cha kutosha na kusisitiza kuendeleza uhusiano wao.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa WFP Kanda ya Kusini mwa Afrika, Dk. Manghestab Haile aliiahidi Serikali ya Tanzania kuendelea kushirikiana na sekta binafsi, kuimarisha masoko na lishe bora kwa raia wake.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Balozi Dk. Pindi Chana, akizungumza na wadau wa chaneli ya utalii ya Tanzania Safari na manaibu mawaziri wa wizara hiyo (hawapo pichani), kuhusu mikakati ya uboreshwaji wa chaneli hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wanaoingiza mifugo vyanzo vya maji waonywa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameonya wananchi wenye tabia ya kuingiza mifugo na kuchoma moto katika chanzo cha maji Mzakwe jijini hapa huku akiagiza watakaobainika wachukuliwe hatua ikiwamo kutozwa faini ya kuanzia Sh. 50,000 hadi 300,000.

Aliagiza upandaji miti katika chanzo hicho ili kuhifadhi eneo hilo ambalo linategemewa kwa kiwango kikubwa kwenye uzalishaji maji.

Mtaka alitoa maagizo hayo jana alipotembelea kukagua chanzo hiko.

Alitaka kutekelezwa sheria ndogo za kulinda chanzo cha maji Mzakwe ambayo ina adhabu kwa wanaoharibu eneo hilo kwa kuingiza mifugo pamoja na kuchoma moto.

Kadhalika, alitaka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) pamoja na uongozi wa Bonde la Maji la Wami-Ruvu kupanda na kutunza miti kwenye eneo hilo.

Alisema hajaridhishwa na hali ya upandaji wa miti katika eneo hilo lenye zaidi ya ekari 4,000, juhudi za upandaji miti zinahitajika ili kulinda chanzo hiko.

"Nawaomba TFS hakikisheni miti inapandwa katika eneo hilo, tunahitaji kuona mazingira ya eneo hili yanakuwa na miti na hali ya kuridhisha," alisema Mtaka.

Alisema suala la mazingira ni muhimu kwa jamii, kila mmoja anapaswa kuwajibika kuhakikisha miti inapandwa katika eneo hilo na kuwa mlinzi wa mwenzake kwenye utunzaji mazingira. Naye, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatuma Mganga, alisema kuna umuhimu wa uratibu mzuri wa utunzaji wa miti katika chanzo hicho, jamii inapaswa kutunza eneo hilo ili lisiharibiwe.

Kwa upande wake, Mstahiki Meya Jiji la Dodoma Prof. Davis Mwamfupe, alisema kuna umuhimu wa ushirikishwaji wa jamii kwenye eneo husika ili kutunza chanzo hiko.

Mhifadhi Misitu Kanda ya Kati, Alexanda Mboya, alisema tatizo linalosababisha miti iliyopandwa kutostawi katika eneo hilo kuwa ni mifugo inayochangia kuharibu mazingira ya eneo hilo.



# Kamati ya Bunge yaomba barabara kupandishwa hadhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, imeagiza barabara inayounganisha Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kupitia katika daraja la Mwasanga kupandishwa hadhi ili kuongeza ufanisi wa usimamizi.

Kamati hiyo imeagiza barabara hiyo kupandishwa hadhi kutoka kusimamiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kwenda Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) kutokana na pia kuunganisha mikoa ya Mbeya na Songwe kupitia Wilaya ya Ileje.

Kamati hiyo ilitoa agizo hilo juzi ilipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa Daraja la Mwasanga ambalo linaunganisha kata tatu za Mwasanga, Tembela na Mwakibete katika Jiji la Mbeya pamoja na baadhi ya Kata za Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Daraja hilo ni lile ambalo lilibomoka mwaka 2019 na kusababisha vifo vya watu watano na kukata mawasiliano kwenye maeneo hayo kwa zaidi ya miaka mitatu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Abdalah Chaurembo, alisema wajumbe wa kamati hiyo waliamua barabara hiyo kupandishwa hadhi kutokana na umuhimu wake katika kusafirisha mazao ya wananchi.

Alisema Daraja la Mwasanga linajengwa kwa kiwango cha TANROADS kutokana na kuwa na uwezo wa kuhimili magari yenye uzito wa zaidi ya tani 20 wakati barabara za TARURA madaraja yake mwisho tani 10.

Alisema daraja haliwezi kuwa na viwango vya TANROADS wakati barabara ina viwango vya TARURA, akasema ni muhimu kuipandisha hadhi ili iwe na kiwango cha aina moja katika maeneo yote.

"Barabara za TARURA viwango vyake ni vya kupitisha magari ya tani 10 na endapo mwananchi atapitisha mzigo mzito zaidi huwa anatozwa faini kubwa kupita kiasi, sasa tunataka barabara hii iwe na viwango sawa na daraja ili kuwaepusha wananchi na faini," alisema Chaurembo.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa alisema alifanya ziara hivi karibuni katika daraja hilo baada ya kusikia malalamiko ya wananchi wa maeneo hayo ili kubaini shida iliyopo.

Alisema baada ya kujionea serikali iliamua kutenga Sh. bilioni 1.4 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hilo upya na aliagiza lianze kujengwa Machi mosi, lakini likaanza Machi 7.

Kutokaana na agizo la Kamati ya Bunge aliamua kumuagiza Mkuu wa mkoa kuanza michakato ya kuipandisha hadhi ili kukidhi mahitaji ya wananchi pamoja na kutekeleza agizo hilo.

"Mchakato wa kupandisha barabara hadhi huanzia kwenye Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) ambayo mwenyekiti wake ni Mkuu wa mkoa, kwa kuwa yupo hapa natumia nafasi hii kumuagiza aanze michakato haraka," alisema Bashungwa.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema barabara hiyo ni miongoni mwa zinazokidhi vigezo vya kupandishwa hadhi kutokana na kuunganisha mikoa miwili.

Homera alisema hivi karibuni aliagiza watendaji wa TANROADS na TARURA, kutembelea barabara zote na kuainisha zinazostahili kupandishwa hadhi ili wawasilishe taarifa kwenye kikao cha RCC kijacho.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa akimjulia hali Cecilia Maglasi, aliyefika katika Hospitali ya Wilaya ya Mbeya jana, kupata matibabu. Bashungwa alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi katika hospitali hiyo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## TARI kuzalisha mbegu mpya za maharagwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Nchini (TARI), kituo cha Uyole jijini Mbeya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo, wamezalisha mbegu mpya za maharagwe ambazo zina uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mbegu hizo zina uwezo wa kuzaa kwa mwingi tofauti na zile za asili na kuwainua wakulima kiuchumi na kuwahakikishia usalama wa chakula.

Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha wadau wa kilimo cha maharagwe kutoka katika mikoa minne ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini cha kutathmini mbegu mpya.

Dk. Bucheyeki alisema mbegu hizo zina uwezo wa kuhimili magonjwa na hali mbaya ya hewa ikiwamo mvua nyingi na hata ukame na kusisitiza kuwa uzalishaji wake hauna gharama kubwa ikilinganishwa na aina zingine.

Alisema mbegu hizo zinaanza kufanyiwa majaribio katika wilaya 10 za mikoa minne ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kabla ya kuanza kusambazwa kwa wakulima wa mikoa mingine.

"Sasa hivi tunaenda kidijitali zaidi, hizi mbegu tunazifanyia tathmini kila mdau kwa njia anazojua yeye, lakini leo tunafanya tathmini ya pamoja ili tuwe na uhakika wa kile tunachowapelekea wakulima," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema kwa sasa kilimo kinahitaji kuwa na teknolojia za kisasa ili kiwe na tija kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa sasa yanaitesa dunia.

# Polisi yataka matukio ya uvunjifu amani kudhibitiwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limewataka viongozi wa kata na vijiji kushirikiana na jeshi hilo kudhibiti matukio ya uvunjifu wa amani ikiwamo mauaji ya watu kwa kuzuia migogoro isiyokuwa ya lazima kwenye jamii.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei alitoa ombi hilo juzi kwenye mkutano maalumu na maofisa watendaji wa kata wa Wilaya ya Mbeya.

Kikao hicho kilikuwa na lengo la kuwatambulisha wakaguzi Kata wa Jeshi hilo waliopangwa kwenye kata zao pamoja na kutoa elimu ya kukabiliana na matukio ya uhalifu kwenye jamii ikiwamo kusuluhisha migogoro kwa haki.

Kamanda Matei alisema lengo la kuwapanga maofisa hao kwenye kata ni utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro la kuongeza nguvu ya kukabiliana na matukio ya uhalifu kwenye jamii.

Alisema kazi ya maofisa hao wa polisi kwenye kamati ni pamoja na kushirikiana na vikundi vya ulinzi shirikishi (Sungusungu) kulinda na kuwadhibiti wahalifu.

"Tunaomba tushirikiane kukabiliana na matukio haya ya uhalifu kwenye maeneo yetu, mkisuluhisha migogoro kwa hali mtasaidia kupunguza matukio haya ya uhalifu kwenye maeneo yenu, ukishindwa kuusuluhisha mgogoro husika unaupeleka ngazi ya juu yako," alisema Kamanda Matei.

Alisema matukio ya uhalifu yanapoongezeka kwenye jamii yanasababisha kukwama kwa shughuli za maendeleo na kusababisha wananchi kuishi kwa hofu. Akizungumza kwa niaba ya Mkuu Wilaya ya Mbeya, Kaimu Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Vincent Mbua, alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kuwapeleka wakaguzi kwenye kata huku akiahidi serikali kushirikiana nao.

Aliwaagiza maofisa watendaji wa kata zote za wilaya hiyo kuhakikisha wanawatafutia wakaguzi hao ofisi za kufanyia kazi ili wafanye kazi kwa uhuru na kwa weledi.

Wakati wa maadhimisho ya siku ya wanawake duniani Machi 8, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alilitaka Jeshi la Polisi kuongeza ushirikiano na wadau katika kukabiliana na uhalifu kwenye jamii.

Aidha, aliwataka viongozi wa dini zote kutoa mafundisho yatakayosaidia kukomesha uhalifu hasa mauaji yanayosababishwa na wivu wa mapenzi.

# TANGAZO

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA: UTOAJI WA HUDUMA ZA MSAADA WA AFYA NA USALAMA KATIKA MRADI WA EACOP KUMBUKUMBU NA. 0010007538

Kampuni ya EACOP LTD ya nchini Tanzania. Inakaribisha mashirika yenye uzoefu na yenye sifa kuonesha nia yao ya UTOAJI WA HUDUMA ZA MSAADA WA AFYA NA USALAMA katika mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilometa 1,443, kati yake kilometa 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA**

- Kutoa Meneja wa HSE aliyemwaminifu, aliyepo Dar es Salaam, mwenye uzoefu wa kutosha wa masuala ya HSE ambaye ataisaidia timu na kuwa kiungo kwa mawasiliano na Chumba cha Udhibiti cha IVMS kilichopo katika Ofisi ya Dar es Salaam kwa lengo la kuhakikisha kuwa timu iliyoko katika eneo la kazi inabaki katika hali ya usalama.
- Kutoa Maafisa kazi wa H&S wenye uwezo na uzoefu kwa kwa ajili ya huduma hizo, kwa kuzingatia vigezo muhimu vya OSHA TZ- NOSHC I na II, wenye uzoefu wa kazi usiopungua miaka 4 katika mazingira yanayofanana na haya; majukumu yake yatakuwa:
- Kusaidia katika utengenezaji wa Mipango ya Usimamizi wa Safari, kwa timu iliyopangwa kwenda eneo la kazi.
- Kuwasiliana moja kwa moja na chumba cha Udhibiti cha IVMS kwa masuala yanayohusiana na Safari.
- Kuendesha majadiliano ya ana kwa ana ya usalama kazini kila asubuhi, kuhakikisha kuwa ukaguzi wote wa magari unafanywa na kushughulikia dosari zote zinabainika, kufanya kazi kwa karibu na Menejimenti ya mkandarasi wa HSE ili kuhakikisha taratibu na maadili ya EACOP yanafuatwa, kuripoti na kuchunguza matukio yote yanayoweza kutokea katika eneo la kazi.
- Kuwapatia Maafisa Usalama wote Kompyuta mpakato za kisasa kwa ajili ya kurekodi Taarifa zote za HSE na Simu za upepo (Setellite Telephone).
- Kumpatia kila Afisa wa HSE simu na muda wa maongezi wa kutosha kila mwezi.
- Kutoa Msimamizi wa HSE atakayesimamia data zote za HSE katika eneo la kazi pamoja na kwenye kanzidata.
- Kufanya ufuatiliaji wa usalama wa malazi mahali pa makazi, Mafunzo ya ukaguzi wa elimu usafi ya HSE (Maelekezo na Mafunzo mengine ya H&S), Kuandaa Mafunzo mahususi ya H&S, Tathmini ya viashiria vya Hatari, (Utambuzi wa JHA NA HATARI), Utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Usalama, Upangaji wa Msaada wa Dharura, Kuandaa majaribio ya utekelezaji wa usalama kwenye eneo la kazi.
- Ripoti ya kila mwezi, fomu ya utendaji kazi, Matukio na ajali pamoja na mipango Madhubuti ya HSE, ikijumuisha hatari zilizobainishwa, mada za usalama n.k.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni/Mashirika yanayoonesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa kusajiliwa kama kampuni ya Ushauri ya HSE kama inavyotakiwa chini ya Sheria ya Tanzania.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Cheti cha Kulipa kodi ya mapato kwa (TRA) cha hivi karibuni.
- Leseni ya kufanya kazi kutoka Tume ya Udhibiti OSHA.
- Maelezo mafupi yanayoonesha uzoefu wa muda usiopungua miaka mitatu katika utoaji wa huduma zinazofanana hizi.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za fedha ya mwaka.
- Wakati wa kuwasilisha majibu ya kuonesha nia, waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamejisajili kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma wa Ndani.
- Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Ushahidi wa taasisi kuhusu usimamizi wa mfumo na sera za HSE, utaratibu na mchakato wa kuzingatia viwango vya ndani na Viwandani vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hizi.
- Leseni stahiki kutoka kwa mamlaka husika za ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma ikiwa ni pamoja na leseni ya biashara, usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na cheti cha hivi karibuni cha mlipa kodi.

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma maombi ya kuonyesha nia yao pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia baruapepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) kabla ya saa **11 :00** jioni kwa saa za Afrika Mashariki (EAT). Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **29 Machi 2022.** Kichwa cha Baruapepe kinapaswa kuwa Kichwa cha Baruapepe kinapaswa kuwa ni **0010007538.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. **Makampuni ya awali yenye vigezo ndiyo yatakayopokea mrejesho.** Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Maombi yote ya kuonyesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza .

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA: UTOAJI WA HUDUMA ZA MAFUTA KWA MAGARI NA VIFAA VINGINE KWENYE MAENEO YA MKUZA WA BOMBA LA MRADI WA EACOP. KUMBUKUMBU Na. 0010007537

Kampuni ya EACOP LTD ya nchini Tanzania Inakaribisha mashirika yenye uzoefu na yenye sifa kuonesha nia yao ya kutoa huduma ya mafuta kwa ajili ya magari na vifaa vingine katika maeneo ya mkuza wa bomba la mafuta katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443 kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA MRADI**

- Mwombaji awe amekidhi vigezo vya Sheria ya OSHA ya Tanzania ya mwaka 2003, pamoja na kuambatanisha na Cheti cha OSHA.
- Kukidhi kiwango cha chini cha mahitaji ya kituo cha mafuta kwa mujibu wa Sheria ya EWURA sura ya 414, na Sheria ya mafuta ya Petroli sura ya 392, ya mwaka 2015 au kama inavyofanyiwa marekebisho mara kwa mara.
- Kuzingatia utunzaji wa mazingira.
- Awe amethibitishwa na kukidhi vigezo vya udhibiti wa majanga ya moto.
- Kuzingatia viwango vya TBS TZS 672: 2012 - EAS 158:2012 ICS 75.160,20; TZS 674: 2012 – EAS 177:2012 ICS 75.160.20: TZS 1076:2008 TZS 1115: 2009.
- Vituo vya mafuta viwe katika maeneo yafuatayo, Muheza, Handeni, Wilaya Kilindi, Kibirashi, Kiteto (Kibaya), Hanang, Chemba, Igunga, Kagongwa, Bukombe (Ushirombo), Chato, Muleba, Misenyi (Mutukula), Kyaka.
- Kituo cha mafuta au kampuni zinazoweza kutoa kwa wateja kadi za kununua mafuta zenye miraba ya sumaku, au misimbo ya kufungulia na nambari ya utambulisho ya siri au nambari ya usalama) zitapewa kipaumbele.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa kusajiliwa kama muuzaji wa mafuta/ Kituo cha mafuta/Kampuni ya mafuta kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Tanzania.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha mlipa kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Leseni ya kufanya kazi kutoka Tume ya Kudhibiti Nishati.
- Maelezo mafupi ya uzoefu katika huduma za kukodisha na matengenezo ya gari.
- Taarifa ya uzoefu inayoonyesha angalau shughuli tatu (3) zinazofanana hizi.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa ya fedha ya mwaka.
- Wakati wa kuwasilisha majibu ya kuonesha nia, waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamejisajili kwenye kazidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani.
- Kukidhi vigezo na Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.
- Ushahidi wa taasisi kuhusu usimamizi wa mfumo na sera za HSE, utaratibu na mchakato kwa kuzingatia viwango vya ndani na Viwandani vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hizi.
- Leseni stahiki kutoka kwa mamlaka husika za ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma.
- Orodha ya wateja watano (5) bora ikijumuisha huduma zitolewazo kwa wateja.
- Cheti cha Usajili (ambatisha nakala).
- Wasifu wa mtu atakayehusika na mawasiliano na upande wa Mradi.

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma maombi ya kuonyesha nia yao pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya tare **29 machi 2022** saa **11 : 00** jioni saa za Afrika Mashariki (EAT). Kichwa cha Baruapepe kinapaswa kuwa ni **0010007537.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. **Makampuni ya awali yenye vigezo ndiyo yatakayopokea mrejesho.** Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Maombi yote ya kuonyesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza .

HABARI KITAIFA

## Mabula ataka ardhi kupewa kipaumbele

**Na Munir Shemweta,** SINGIDA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka wananchi kuipa kipaumbele sekta ya ardhi kwa kuwa ikitumiwa vizuri itawezesha kuchochea mapinduzi kiuchumi.

Pia amewataka wananchi na taasisi zote zinazomiliki ardhi nchini kuhakikisha zinatimiza wajibu wa kulipa kodi ya pango la ardhi kila mwaka kwa maendeleo endelevu.

Dk. Mabula alisema hayo juzi wakati wa utoaji hatimiliki za kimila kwa wananchi wa wilaya ya Ikungi. Zaidi ya hati 5,050 zimeandaliwa kupitia mradi wa matumizi ya ardhi uliotekelezwa kwa pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Wanawake (UN Women) na Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Korea (KOICA).

"Mimi na wizara yangu tunaamini kuwa ardhi ikitumiwa vyema kwa maana ya kupangwa, kupimwa na kumilikishwa, itawezesha kuchochea mapinduzi makubwa na ya haraka ya kiuchumi kwa mwananchi mmoja mmoja kwenye mikoa yetu na taifa kwa ujumla," alisema.

Waziri Mabula aliwaambia wananchi wa Ikungi waliopokea hati katika hafla hiyo kuwa wamenufaika kwa kupata nyaraka ya kumiliki ardhi alizozieleza kuwa zina faida kubwa katika maisha yao ya kila siku.

Alitaja baadhi ya manufaa hayo kuwa ni usalama wa miliki za ardhi, uhakika wa milki, kupunguza migogoro na kutumia hatimiliki kama dhamana katika taasisi mbalimbali kama vile za fedha, vyombo vya kisheria sambamba na kupandisha thamani ya ardhi.

"Nitoe rai kwa wananchi wote kuwa na tabia ya kutumia na kuchangamkia fursa kama hizi zinapotokea katika maeneo yetu ili kupata manufaa kama haya" alisema.

# Wanafunzi Afrika wasimulia adha fursa za vita Ukraine

**Na Waandishi Wetu**

IKIWA ni wiki ya tatu tangu mashambulizi ya Russia dhidi ya Ukraine yaibuke, baadhi ya wanafunzi kutoka nchi za Afrika, ikiwamo Tanzania, wamepata fursa ya kuendelea na masomo yao kwenye nchi za Umoja wa Ulaya (EU).

Licha ya kupata nafasi za masomo, wanafunzi hao bado wanakabiliwa na uhaba wa fedha za kujikimu baada ya kusitishwa huduma kutoka kwa wafadhili wao kimataifa na wazazi au walezi.

Rais wa Wanafunzi kutoka nchi za Afrika nchini Russia, Talo Harrison, alisema juzi kuwa fedha ni kikwazo kwao na kwamba yeye binafsi amebakiza miezi minne ili kuhitimu masomo yake kisha arejee nchini kwao, Kenya.

"Ninasimamia wanafunzi hapa Moscow, shida kubwa waliyo nayo wanafunzi ni hofu kwa kuwa wanafunzi hawajui nini kitafanyika kesho kwa sababu hawawezi kupata fedha kutoka nyumbani na wengine walikuwa wanafanya kazi kutoka kampuni za kimataifa, lakini sasa hakuna.

"Hawana pesa ya matumizi, chakula, hawajui watapataje pesa kutoka kwa wafadhili au wazazi. Hofu yao ni hiyo watapata wapi pesa za kujikimu hali inakuwa ngumu. Nina wasiwasi hata mimi natamani kurudi nyumbani, ila nikiondoka sasa hivi, kilichonileta huku ni kusoma lazima nimalize ndipo nirudi. Unakuta mtu amesomea miaka mitano, ukisema urudi nyumbani ni changamoto, inabidi uvumilie," alisema Harrison.

Alisema baada ya kumalizika janga la Uviko-19 lililowaathiri wanafunzi kisaikolojia kutokana na sharti la kukaa ndani, kuwapo kwa vita hivi sasa kumewaongezea tatizo la afya ya akili.

### KUSOMA VYUO ULAYA

Wakati hali ikiwa hivyo, nchi za EU zimetoa fursa kwa wanafunzi waliotoka Ukraine kwa sababu ya vita kuendelea na masomo katika vyuo vilivyoko katika nchi hizo.

Mmoja wa wanafunzi wa Kitanzania waliokuwa wanasoma Ukraine na kukimbilia mji wa Budapest, Hungary kutokana na vita vinavyoendelea, amethibitisha hayo alipokuwa akihojiwa na chombo kimoja cha habari.

Alisema wako takribani wanafunzi wa Kitanzania 100 katika mji wa Budapest, ambao wanatafuta vyuo kutokana na kuruhusiwa kuendelea na masomo katika nchi za EU.

"Tuko katika makundi tofauti. Kuna wale ambao wanataka kuhama kwa sababu tumepewa fursa ya kuendelea na masomo katika nchi za Ulaya, kwa hiyo kuna wengine wanakwenda Ujerumani, Italia na wengine wanabaki hapa hapa Hungary," alisema.

Pia alisema walifanikiwa kuingia nchini humo kutoka mji wa Sumy, hivyo kuishukuru serikali kupitia ubalozi wake nchini Ukraine kwa msaada waliotoa kwao.

"Tulikuwa tunafanya mawasiliano (ubalozi) nao kwa muda wote tuliokuwa kwenye matatizo na wali-play big part' kutusaidia ingawa njia waliyokuwa wanaitumia ni ya Russia kwa sababu tulikuwa karibu na njia hiyo," alisema.

Akizungumzia walivyofanikiwa kutoka Ukraine, mwanafunzi huyo alisema mwanzoni ilikuwa vigumu kwa sababu walikuwa wamezingirwa na majeshi ya Russia.

***Imeandikwa na Christina Mwakangale na Jenifer Gilla***




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (wapili kulia), akipokea msaada wa madawati 100 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 20 kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano Benki ya Exim, Stanley Kafu, jijini Mbeya jana, ikiwa ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo wa kutoa madawati 1,000 katika mikoa mbalimbali hapa nchini, ili kuchangia utoaji wa elimu bora kupitia mpango wake wa uwajibikaji wa jamii, ujulikanao Exim Cares. Kulia ni Katibu Tawala wa Mkoa huo, Angelina Lutambi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ sasa kukusanya mapato kidijitali

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), kupitia Wakala wa Serikali Mtandao ('eGovernment Zanzibar) na Benki ya NMB, wamesaini makubaliano ya ushirikiano, yatakayowezesha mifumo ya benki hiyo kuingiliana na ZanMalipo na kuwezesha taasisi za SMZ, kukusanya mapato kupitia matawi na mifumo ya kidijitali.

Hafla ya kusaini makubaliano hayo imefanyika mjini hapo jana na benki hiyo imesema imejipanga kuimarisha ushirikiano huo ambao utakuwa chachu ya ukuaji wa uchumi visiwani humo na kwamba inaamini utakuwa wa karibu zaidi, endelevu na wenye manufaa kwa SMZ na taasisi zake, utakaoleta maendeleo chanya.

Akizungumza kabla ya kusaini makubaliano hayo ya mwaka mmoja yenye kipengele kinachoruhusu mazungumzo na kuyarefusha, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alipongeza SMZ chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa mageuzi chanya ya kiuchumi yanayochakatwa na kusimamiwa na serikali yake kwa ustawi wa taifa.

Zaipuna alisema makubaliano hayo ni chachu kwa taasisi yake kubuni suluhishi mbalimbali za Wazanzibar na taifa na kwamba maendeleo ya kidijitali kwa ulimwengu wa sasa hayaepukiki, ushirikiano wao huo utakuwa na mchango chanya katika kuharakisha ukuzaji uchumi na kurahisisha utendaji wa serikali.

"Makubaliano haya ni kielelezo tosha kuwa Serikali ya Zanzibar na NMB sasa tunaenda kushirikiana kuboresha huduma za ukusanyaji mapato na malipo, sambamba na kuwezesha mifumo yetu kuingiliana na ile ya ZanMalipo, kuwezesha Taasisi za SMZ kukusanya mapato kupitia matawi ya NMB na mifumo ya kidijitali ya benki yetu.

"Kupitia makubaliano haya, NMB na eGovenment Zanzibar, tunaenda kutengeneza Kituo cha Pamoja cha Malipo Kidijitali 'One Stop Center,' cha Shirika la Bandari Zanzibar, ambacho kitampa mlipaji wa huduma mbalimbali 'control number' moja kwa ajili ya kufanyia malipo mbalimbali bandarini, badala ya namba tofauti.

"Suluhisho hizi mbili zinazoambatana na makubaliano haya, zinaenda kuboresha utoaji huduma kwa wananchi, lakini kuongeza ufanisi katika ukusanyaji mapato na kuondoa kero ya muda mrefu wanaotumia wananchi kufanya huduma za malipo," alisisitiza Zaipuna mbele ya wanahabari katika Ukumbi wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Alibainisha kuwa, SMZ kupitia eGovernment na NMB, wanaenda kujenga ushirikiano utakaokuwa chachu ya ukuaji wa uchumi na matarajio yao ni kuwa na ushirikiano endelevu wa karibu zaidi, wenye manufaa kwa SMZ na taasisi zake, utakaoleta maendeleo chanya ya serikali, taifa na wananchi kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa eGovernment Zanzibar, Said Seif Said, aliishukuru NMB kwa kusaini makubaliano ya ushirikiano huo, ambao aliutaja kama mwarobaini wa changamoto mbalimbali za kimalipo wanazokutana nazo wananchi wa Zanzibar, unaoenda pia kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato ya serikali.

"Sisi eGovernment tunaamini kwamba ushirikiano huu ni chanya, utakaobeba tija kwa serikali, hususani hiyo 'One Stop Center' ambayo itajikita katika kurahisisha mifumo ya malipo bandarini ambako tutatumia mifumo ya kidijitali kuongeza ufanisi kwenye makusanyo mbalimbali.

# BANDA NA MALAWI KUKIPIGA UTURUKI, CHAMA NA WASAUZI

**Na Mwandishi Wetu**

WINGA wa Simba, Peter Banda atakuwa nchini Uturuki kwa muda wa siku tano akiitumikia timu yao ya Taifa ya Malawi chini ya miaka 23 kwenye michuano ya Antalya Cup.

Banda na nyota wawili wa Zambia Clatous Chama na Rally Bwalya wameitwa kuzitumikia timu zao za taifa katika kipindi hiki ligi mbalimbali duniani zikisimama kupisha Kalenda ya Fifa.

Chama na Bwalya wameitwa kwenda kuitumikia Zambia 'Chipolopolo' katika mechi mbili za kirafiki dhidi ya Afrika Kusini na Guinea zitakazopigwa Machi 25 na 29, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na uongozi wa Klabu ya Simba, wachezaji hao watajiunga na timu zao za taifa baada ya mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast itakayopigwa Jumapili wiki hii nchini Benin.

**Mechi hiyo inapigwa Benin kutokana na viwanja nchini Ivory Coast kuwa katika ukarabati mkubwa kwa ajili ya fainali zijazo za Afcon.**

"Nyota wetu watatu wa kimataifa wameitwa katika timu zao za taifa wakati ligi zikisimama kupisha mechi za Kalenda ya Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), nyota hao ni Clatous Chama, Rally Bwalya na Peter Banda," ilieleza taarifa hiyo.

Simba ambayo inaongoza Kundi D ikiwa na pointi saba, inatarajia kuifuata Asec Mimosas Ijumaa wiki hii kwenye mechi hiyo ambayo kama ikishinda itakuwa imejihakikishia tiketi ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo ya Afrika.

Katika kundi hilo ambalo kila timu imebakiza michezo miwili, Asec Mimosas na RS Berkane ya Morocco kila moja ina pointi sita huku US Gendamarie ya Niger ikiburuza mkia kwa alama zake nne.

Endapo Simba itashinda Jumapili itafikisha pointi 10 ambazo zinaweza kufikiwa na Berkane kama nayo itashinda Jumapili dhidi ya US Gendamarie na kisha kushinda mchezo wake wa mwisho ama kupata sare dhidi ya Asec Mimosas.

Lakini US Gendamarie nayo inaweza kumaliza na alama 10 kama ikishinda dhidi ya RS Berkane Jumapili na kisha kushinda mchezo wake wa mwisho dhidi Simba katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Aprili 3, mwaka huu..


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

KUMBUKIZI YA MWAKA MMOJA WA KIFO CHA JPM 17 MACHI, 2022

*Bodi ya wakurugenzi, menejimenti na watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), leo tunaadhimisha mwaka mmoja tangu ututoke hapa duniani Rais wa awamu ya tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hayati Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.*



*Pumzika kwa amani!*

John Pombe Magufuli 1959 - 2021


# Kocha Biashara apasua kichwa kuibakisha Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Vivier Bahati, amesema anapambana kuisuka timu yake kuwa imara na kupata matokeo mazuri kwa lengo la kujihakikishia msimu ujao wanaendelea kuwapo kwenye Ligi Kuu Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili jana, Vivier alisema ligi imekuwa ngumu na ushindani mkubwa, lakini atapambana kuhakikisha wachezaji wake wanakuwa makini uwanjani ili kupata matokeo chanya.

Alisema kinachomuumiza kichwa kwa sasa si lingine zaidi kuona kila siku akipata matokeo mazuri ili kufikia malengo ambayo amekubaliana na uongozi wake ya kuibakisha timu hiyo Ligi Kuu msimu ujao.

"Nafurahi kuona mabadiliko makubwa kwa timu yangu tofauti na nilipoikuta, sasa hivi nina matarajio makubwa ya kupata matokeo mazuri katika kila mechi," alisema Vivier.

Alisema kwa sasa hafikirii zaidi nafasi za juu sana zaidi ya kuhitaji kuona timu yake hiyo inafanikiwa kupata pointi muhimu katika kila mechi ili kutimiza malengo yanayotarajiwa ya kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Biashara United imeshacheza michezo 18 ikishinda mitatu tu, sare 10 na kupoteza mechi tano, hivyo kujikusanyia pointi 19 zinazoiweka katika nafasi ya 13, kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

# 600 wajitokeza kushiriki Tanga City Marathon

**Na Cheji Bakari,** TANGA

ZIKIWA zimebaki siku 10 tu, kabla ya mashindano ya kimataifa ya mbio za Nusu Marathon ya Tanga City Marathon Season 6, kuanza kutimua vumbi jijini hapa, tayari idadi ya washiriki 600 wameshajiandikisha kushiriki mbio hizo.

Mwandaaji wa mbio hizo, Juma Mwajasho, akizungumza na mwandishi wetu jana, alisema kadri muda unavyosonga mbele ndivyo idadi ya washiriki inaongezeka kwa kasi.

"Idadi ya washiriki waliojiandikisha kushiriki mbio hizi kwa wiki hii, imeongezeka kwa kasi kubwa sana kutoka watu 150 hadi 600 na bado wengine wanaendelea kuongezeka," alisema.

Mashindano hayo ya mbio za kilometa 21, 10 na tano, ambayo yanashirikisha washiriki kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania pamoja na nchi jirani za Afrika Mashariki, yanatarajiwa kutimua vumbi Machi 27, mwaka huu jijini Tanga huku mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima.

## ZISIKUPITE

### HAALAND NA MASHARTI

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund na Norway Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, ataomba kiwekwe kipengele cha kumruhusu kuondoka kwenye mkataba wowote atakaoingia kama atabadili klabu msimu ujao. (***Sun***)

### SUAREZ MSIMU MMOJA

NYOTA wa Atletico Madrid, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 35, anataka kucheza angalau msimu mwingine mmoja Ulaya kabla ya kutimkia Ligi Kuu ya Matekani, MLS. (***Mail***)

### CALLYER ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imekubali kumsajili kiungo mwenye miaka 18, Toby Collyer kutoka Brighton. (***Mirror***)

### KESSIE, CHRISTENSEN MILAN

KIUNGO wa AC Milan kutoka Ivory Coast, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 25, atakuwa usajili wa kwanza wa Barcelona katika dirisha la majira ya joto litakapofunguliwa, huku beki wa kati wa Chelsea, Andreas Christensen mwenye miaka 25 akifuata. (***ESPN***)

### KANE KUBAKI SPURS

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane mwenye miaka 29, amesema "anachagizwa kuwa bora zaidi" chini ya kocha, Antonio Conte, licha ya tetesi za mpango wa kutimkia Manchester United. (***Sky Sports, via Mirror***)

### MADRID, ARSENAL KWA RUIZ

ARSENAL inakabiliana na upinzani mkali kutoka Real Madrid na Barcelona kwa ajili ya kiungo wa Napoli, Fabian Ruiz mwenye umri wa miaka 25. (***Corriere dello Sport, via Express***).

### NEVES AMULIKWA BARCA

KLABU ya Barcelona itamuwania kiungo wa Wolves, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25, kama mbadala wa nyota wake wa kimataifa wa Hispania, Sergio Busquets mwenye miaka 33. (***Mundo Deportivo***)

### ARSENAL KUONGEZA DAU

KLABU ya Arsenal imeongeza akiba yake kwa pauni milioni 20 kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji mpya baada ya kumuuza kiungo Matteo Guendouzi mwenye umri wa miaka 22 kwenda Marseille, na kiungo wa Uruguay, Lucas Torreira mwenye miaka 26 kwenda Fiorentina. (***Mirror***)

### CESAR KUONDOKA CHELSEA

BARCELONA ina matumaini kwamba Chelsea itamruhusu mlinzi wake Cesar Azpilicueta mwenye miaka 32 kuondoka Stamford Bridge bure msimu huu. (***ESPN, via Express***)

### UNITED YATAKIWA KUSAJILI

MLINZI wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand anaamini klabu hiyo ya Old Trafford inapaswa kujaribu kumsajili mlinzi wa kati wa Paris St-German, Marquinhos mwenye umri wa miaka 27. (***MEN***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MO SALAH SASA ANUKIA KUONDOKA BURE LIVER

**Hakuna maendeleo zaidi juu ya mazungumzo ya mkataba mpya na hiyo inaweza kuchochea yeye...**

**LIVERPOOL,** ENGLAND

MOHAMED Salah bila shaka ndiye mchezaji bora zaidi duniani kwa kiwango cha sasa, ingawa Liverpool bado hawajamfunga kwenye mkataba mpya.

Mazungumzo kuhusu masharti mapya kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, yamekuwa yakiendelea kwa muda, lakini hakuna kinachokaribia kuafikiwa.

**Pamoja na mkataba wake kuelekea kumalizika mwa ka 2023, Salah anaweza kuwa mmoja wa wachezaji watakaoondoka bure mwishoni mwa msimu huu.**

Kwa mujibu wa mwandishi mashuhuri wa habari za michezo wa Italia, Fabrizio Romano, Salah ana furaha tele ndani ya Liverpool na hafikirii kuhama kwenda kwa miamba ya Hispania, Real Madrid au Barcelona.

Hata hivyo, kumekuwa hakuna maendeleo zaidi juu ya mazungumzo ya mkataba mpya na hiyo inaweza kuchochea yeye kuondoka.

Salah, ambaye tayari amefunga mabao 28 msimu huu katika mashindano yote, bado anaelekeza nguvu zake zote kwa Liverpool, lakini anaweza kuondoka bila malipo mwishoni mwa msimu ujao.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,042

MECHI KALI
WEST HAM
VERSUS
SEVILLA FC
1 | 2.20
X | 3.31
2 | 3.31

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ‘MBAPPE, HAALAND HAWATAIBADILISHA MANCHESTER UTD’

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe na Erling Haaland hawataweza kubadilisha chochote ndani ya Manchester United, kwa mujibu wa gwiji wa zamani wa ‘Mashetani Wekundu’ hao, Rio Ferdinand.

United walilazwa na kuondolewa katika hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi na Atletico Madrid, ambao ushindi wao wa bao 1-0 ugenini pale Old Trafford uliifanya timu ya Diego Simeone kushinda kwa jumla ya mabao 2-1, juzi Jumanne.

Hiyo ilimaanisha kwamba United wameshindwa kufuzu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu 2011, waliposhindwa na Barcelona katika mchezo wa fainali uliopigwa Wembley chini ya Alex Ferguson.

Hali ya kupoteza kwa Atleti ilileta mwelekeo mkali, lakini Ferdinand anaamini mabadiliko zaidi ya kimfumo katika klabu ni muhimu, tofauti na uwekezaji wa kikosi.

Ralf Rangnick atabakia kuifundisha United kwa muda hadi mwishoni mwa msimu huu, na Ferdinand anataka kuona kocha akiletwa ambaye anaweza kuleta mafanikio na kuwaondoa Mashetani Wekundu katika kipindi kigumu.






# *Ukraine yapewa tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia*

**NYON,** Uswisi

TIMU ya Taifa ya Ukraine itakwenda kushiriki michuano ya Kome la Dunia moja kwa moja kama ilivyothibitishwa na Chama cha Soka nchini Wales kuwa mazungumzo yamefanyika na Shirikisho la Soka la Kimataifa, FIFA.

Scotland ilipaswa icheze na Ukraine Machi 24, mwaka huu, kwenye kuwania kufuzu kucheza Kombe la Dunia nchini Qatar, lakini mchezo uliahirishwa hadi Juni kutokana na uvamizi wa Urusi, wakati Wales na Austria mchezo wao watacheza kama ulivyopangwa.

Mkurugenzi wa Chama cha Soka nchini Wales, Paul Mooney, alisema “ilikuwa wazo la Wales kama tungeweza kulifanya hili ingekuwa kitu kizuri kufanya, ni jambo kama binadamu ungesema sawa, kama hawataweza kucheza Juni inabidi wapewe nafasi kuingia moja kwa moja.

“Kulikuwa na mwanya wa mazungumzo haya, kusema kungepatikana nafasi ya ziada kwa Ukraine, kwa sababu ya mambo ya kutisha yanayoendelea kwao, lakini tunamaanisha nafasi ya ziada kwenye Kombe la Dunia, kama huku zikibaki tatu, sisi wenyewe, Scotland na Austria na kitu kikubwa kwetu ni kushiriki Kombe la Dunia.



## HABARI MICHEZO


# 2,431,860 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/03/22 | 18:00 | Huddersfield vs Bournemouth | 2.51 | 3.29 | 2.65 |
| 02. 19/03/22 | 18:00 | Reading vs Blackburn | 2.60 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 19/03/22 | 18:15 | Eupen vs Mechelen | 2.76 | 3.40 | 2.39 |
| 04. 19/03/22 | 20:45 | GO Ahead Eagles vs Cambuur | 2.48 | 3.45 | 2.70 |
| 05. 19/03/22 | 23:00 | Nantes vs Lille | 2.87 | 2.97 | 2.63 |
| 06. 20/03/22 | 14:30 | Venezia vs Sampdoria | 2.55 | 3.35 | 2.70 |
| 07. 20/03/22 | 15:30 | Jahn Regensburg vs Paderborn | 2.75 | 3.24 | 2.45 |
| 08. 20/03/22 | 16:00 | Gaziantep BB vs Galatasaray | 2.71 | 3.36 | 2.45 |
| 09. 20/03/22 | 17:00 | Bordeaux vs Montpellier | 2.40 | 3.45 | 2.80 |
| 10. 20/03/22 | 17:00 | Empoli vs Verona | 3.20 | 3.40 | 2.20 |
| 11. 20/03/22 | 18:00 | Ponferradina vs Eibar | 2.50 | 3.09 | 2.80 |
| 12. 20/03/22 | 18:15 | Celta Vigo vs Betis | 2.41 | 3.34 | 2.89 |
| 13. 20/03/22 | 20:00 | Roma vs Lazio | 2.34 | 3.41 | 2.96 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 17/03/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3677 | Dong Tam Long AN vs PHO Hien FC | 1.98 | 2.93 | 3.94 |
| 14:00 | 3308 | FK Arys vs FK Kaspiy Aktau | 2.74 | 2.98 | 2.50 |
| 14:00 | 3756 | Ordabasy vs Akzhaiyk Uralsk | 2.29 | 3.09 | 2.94 |
| 14:00 | 5881 | Kairat Almaty vs Taraz | 1.37 | 4.34 | 7.14 |
| 14:30 | 3730 | Aluminium Arak vs Teraktor Sazi | 2.04 | 2.56 | 4.55 |
| 15:00 | 2280 | Vihiga Bullets FC vs Nzoia United | 4.34 | 2.94 | 1.89 |
| 15:00 | 2325 | Bandari vs Nairobi City Stars FC | 2.46 | 2.75 | 3.04 |
| 15:00 | 4669 | Mathare United vs Posta Rangers | 4.82 | 3.23 | 1.72 |
| 16:00 | 1552 | Astana vs Aktobe | 1.52 | 3.86 | 5.40 |
| 16:00 | 2199 | PAOK Thessaloniki B vs AO Trikala | 1.54 | 3.62 | 5.79 |
| 16:00 | 3869 | Farco FC vs National Bank | 2.67 | 2.48 | 3.37 |
| 16:00 | 5807 | Tobol Kostanay vs FK Kyzylzhar Petropavlovsk | 1.46 | 3.85 | 6.36 |
| 16:30 | 3041 | Navbahor Namangan vs Kokand 1912 | 2.05 | 3.15 | 3.95 |
| 16:30 | 3271 | Persija Jakarta vs Persepam MU | 3.28 | 3.18 | 2.08 |
| 16:30 | 3369 | Sepahan Esfahan vs Gol Gohar | 1.96 | 2.79 | 4.34 |
| 16:30 | 3683 | Triestina vs US Pergolettese | 1.78 | 3.47 | 4.56 |
| 16:30 | 4416 | Foolad Khuzestan vs Fajr Sepasi | 1.67 | 2.99 | 5.99 |
| 17:00 | 2292 | Persepolis FC vs Esteghlal Tehran | 2.24 | 2.75 | 3.47 |
| 18:00 | 2929 | Queretaro U20 vs Atletico San Luis U20 | 5.19 | 3.94 | 1.53 |
| 18:30 | 2858 | Eastern Company SC vs Talaea El Gaish | 3.49 | 2.81 | 2.31 |
| 18:45 | 3258 | Al Faisaly (KSA) vs Al Fateh (KSA) | 2.21 | 3.56 | 2.97 |
| 18:55 | 1651 | Dhamk vs Al-Ettifaq | 2.52 | 3.36 | 2.67 |
| 20:00 | 2074 | Giana Erminio vs Feralpisalo | 4.54 | 3.21 | 1.86 |
| 20:00 | 3025 | SC Kfar Qasem vs Beitar Tel Aviv Ramla | 1.58 | 3.82 | 5.75 |
| 20:45 | 2403 | AZ Alkmaar vs Bodo Glimt | 1.65 | 4.19 | 4.69 |
| 20:45 | 2892 | Rennes vs Leicester | 1.94 | 3.65 | 3.70 |
| 20:45 | 3359 | Galatasaray vs Barcelona | 7.43 | 4.64 | 1.41 |
| 20:45 | 3622 | Red Star Belgrade vs Rangers | 2.17 | 3.50 | 3.20 |
| 20:45 | 4185 | FC Basel vs Marseille | 3.21 | 3.61 | 2.12 |
| 20:45 | 4844 | Monaco vs Sporting Braga | 1.52 | 4.31 | 5.82 |
| 20:45 | 5375 | Bayer Leverkusen vs Atalanta | 2.32 | 3.69 | 2.80 |
| 20:45 | 5773 | Copenhagen vs PSV Eindhoven | 3.35 | 3.75 | 2.02 |
| 20:50 | 1156 | Al Nasr Riyadh vs AL Faiha | 1.27 | 5.55 | 9.90 |
| 21:00 | 5611 | Necaxa W vs Toluca W | 2.45 | 3.36 | 2.54 |
| 21:00 | 5718 | CD Acero vs Recambios Colon CD | 1.46 | 3.66 | 7.13 |
| 21:05 | 4655 | Sacachispas FC vs Independiente Rivadavia | 3.00 | 2.61 | 2.61 |
| 21:30 | 3364 | Siegen vs TSG Sprockhovel | 2.06 | 3.57 | 2.99 |
| 21:30 | 3549 | SE Juventude MA vs SAO Jose MA | 2.38 | 3.00 | 3.25 |
| 22:00 | 5750 | 1. FC Duren vs Siegburger SV 04 | 1.34 | 5.60 | 7.80 |
| 22:45 | 2362 | Lions Gibraltar vs Lynx FC | 6.20 | 4.84 | 1.37 |
| 22:45 | 2902 | Everton vs Newcastle | 2.34 | 3.29 | 3.04 |
| 23:00 | 1522 | Llaneros FC vs Deportes Quindio | 2.56 | 2.95 | 2.70 |
| 23:00 | 1951 | KAA Gent vs PAOK | 1.68 | 3.69 | 5.19 |
| 23:00 | 2592 | Eintracht Frankfurt vs Betis | 2.22 | 3.64 | 2.99 |
| 23:00 | 2900 | Feyenoord vs Partizan | 1.40 | 4.88 | 6.97 |
| 23:00 | 3089 | LASK Linz vs Slavia Prague | 2.43 | 3.50 | 2.75 |
| 23:00 | 4261 | Lyon vs Porto | 2.25 | 3.60 | 2.95 |
| 23:00 | 4913 | Roma vs Vitesse Arnhem | 1.52 | 4.31 | 5.82 |
| 23:00 | 5153 | West Ham vs Sevilla FC | 2.20 | 3.31 | 3.31 |
| 23:05 | 3674 | CA Atlanta vs Almirante Brown | 3.32 | 2.84 | 2.24 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# AISHA WA YANGA PRINCESS KUKIPIGA LIGI KUU SWEDEN

**Na Shufaa Lyimo**

MSHAMBULIAJI kinara wa Yanga Princess, Aisha Masaka, amelamba 'dume' baada ya kusajiliwa na Klabu ya BK Hacken FF inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Sweden.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Klabu ya Yanga, nyota huyo ambaye ni mwiba mkali katika anga za kucheka na nyavu, amesajiliwa kwa makubaliano maalum ambayo hata hivyo haikuyaweka wazi.

"Klabu ya Yanga inamtakia kila la kheri mshambuliaji Aisha Masaka ambaye amesajili na Klabu ya BK Hacken FF inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Sweden," ilieleza taarifa hiyo.

BK Hacken FF ni Mabingwa wa Ligi Kuu Wanawake Sweden msimu wa 2020 na wamekuwa wakishiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa Wanawake na mwaka huu wametolewa na timu ya Wanawake ya Manchester City kwenye michuano hiyo. Akizungumzia usajili huo, Msemaji wa Yanga, Haji Manara alisema mchezaji huyo ameipa heshima kubwa klabu yao kwa kufanikiwa kutoa mchezaji kwenda kucheza soka la kulipwa Ulaya.

"Aisha ametupa heshima si rahisi kwenda kucheza moja kwa moja Sweden bila kufanyiwa majaribio," alisema Manara.



# Msuva awatuliza mashabiki Stars

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Simon Msuva, ameonyesha kufurahishwa kuchaguliwa kwenye kikosi hicho na amewatoa hofu watu wote ambao wamekuwa na mashaka na kiwango chake kwa sababu hana timu kwa sasa, akidai kuwa watamuona Simon yule yule wanaomfahamu kwa sababu bado anafanya mazoezi kama kawaida.

Baadhi ya mashabiki wa soka nchini na wachambuzi wameonekana kumshangaa Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Kim Paulsen, kumwita Msuva ambaye kwa muda sasa hayupo kwenye timu yake ya Wydad Casablaca ya Morocco, wakidai hawezi kuwa kwenye kiwango chake cha kawaida kilichozoeleka.

"Ni jambo jema kuwapo kwenye timu ya taifa, si rahisi kama huchezi kwenye timu halafu unaitwa kwenye kikosi cha timu ya taifa, lakini kwangu mimi nahesabu kuwa timu ninayo, ila nina tatizo na timu yangu, lakini bado ni mchezaji wa timu hiyo, labda kwa sababu sichezi.

# Michezo

Alhamisi Machi 17, 2022

Nipashe




Salah anukia kuondoka bure Liver UKURASA 21

WATAKIONA...



Wachezaji Simba, Pape Sakho (wa kwanza) na Shomari Kapombe wakifanya mazoezi juzi kujiandaa na mechi yao ya marudiano ya Kundi D Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Asec Mimosas itakayopigwa Jumapili wiki hii nchini Benin. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA YAPANIA REKODI MPYA CAF

Kuifuata Asec Mimosas Ijumaa, lakini kikosi kazi chatangulia Benin kuweka mambo sawa huku...

**Na Saada Akida**

WAWAKILISHI pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba, wamepania kuendelea kuandika rekodi mpya kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika wakati huu wakijiandaa kuifuata Asec Mimosas ya Ivory Coast Ijumaa wiki hii.

**Ikumbukwe Simba hii ni mara ya kwanza kushiriki Kombe la Shirikisho Afrika na kutinga hatua ya makundi tangu ianze kuchezwa kwa mfumo mpya wa mtoano kwa mechi za awali na kisha hatua ya makundi.**

Simba iliwahi kufika hadi fainali ya michuano hiyo mwaka 1993 wakati ikichezwa kwa mfumo wa mtoano mwanzo mwisho, na kisha kupoteza mechi hiyo ya fainali dhidi ya Stella Club d'Adjamé ya Ivory Coast, hivyo kwa msimu huu kutinga hatua ya makundi tu ni rekodi mpya kwao.

Hata hivyo, uongozi wa Klabu ya Simba umepania kuendelea kuandika rekodi mpya katika michuano hiyo ya Shirikisho Afrika kwa kwenda sasa kufuzu hatua ya robo fainali ugenini wakati watakapoivaa Asec Mimosas kwenye mechi ya Kundi D itakayopigwa Uwanja wa Felix Houphouet Beigny nchini Benin.

Asec Mimosas imelazimika kutumia uwanja huo wa Benin katika mechi zake zote za nyumbani kutokana na viwanja nchini Ivory Coast kuwa katika ukarabati mkubwa kwa ajili ya michuano ya Afcon ijayo.

Kuelekea mechi hiyo itakayopigwa Jumapili wiki hii, licha ya Simba kutarajia kuondoka Ijumaa, tayari imetanguliza 'kikosi kazi' chake kwenda kuandaa taratibu zote kwa ajili ya timu hiyo ikiwa ni pamoja na sehemu itakaposhukia na uwanja wa mazoezi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi kimeingia kambini kwa ajili ya maandalizi ya mchezo huo na kinatarajia kuondoka saa tisa usiku na ndege ya Shirika la Ndege la Ethiopia wakiwa na kikosi cha wachezaji 24, benchi la ufundi na viongozi wa klabu hiyo.

Alisema kikosi kipo vizuri ikiwamo nahodha wao John Bocco ambaye ameanza mazoezi ya gym ili kujiweka sawa baada ya kupona majeraha yaliyokuwa yanamsumbua.

"Bocco anaendelea vizuri ameanzia gym baada ya hapo ataanza taratibu mazoezi ya uwanjani pamoja na wachezaji wenzake, maandalizi ya mchezo wa marudiano dhidi ya Asec Mimosas yanaendelea vizuri," alisema na aliongeza;

"Tutataingia katika mchezo huo tukiwa na lengo la kutafuta alama tatu muhimu ili kujihakikishia nafasi ya kuingia robo fainali ya michuano hiyo.

"Benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Pablo Franco linaendelea kujiimarisha na kikosi chake kwa ajili ya mchezo wetu huo muhimu ili kupata pointi muhimu na kurejea nyumbani na alama 10.

"Hii ni kutoka na wachezaji na benchi la ufundi kufahamu umuhimu na ugumu wa mchezo huo ambao tunahitaji kutafuta pointi muhimu ili kuendelea kuongoza kundi letu," alisema Ahmed.

## Yanga kuchangia damu mwaka mmoja wa Rais Samia

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Yanga Ijumaa wiki hii itaungana na mashabiki pamoja na wanachama wake kwenda kuchangia benki ya damu katika Hospitali ya Muhimbili jijini Dar es Salaam, kama sehemu ya maadhimisho ya mwaka mmoja wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Msemaji wa klabu hiyo, Haji Manara (pichani), alisema watafanya zoezi hilo kwa vitendo ili kuungana na Rais Samia kuadhimisha mwaka wake huo.

"Kuelekea maadhimisho ya mwaka mmoja wa Rais Samia, kesho (leo), wanachama wa Yanga tutaungana kwa pamoja kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili kuichangia benki ya damu ili kumsaidia rais, sisi tupo kwa ajili ya jamii," alisema Manara.



Alisema wanachama 200 wa kwanza watakaowahi siku hiyo kila mmoja atapatiwa jezi ya Yanga, na kuwataka wanachama wa matawi yote nchini kuungana kwenda kwenye hospitali zao kuchangia damu.

Mbali na hilo, alisema Jumamosi ya wiki hii watafanya usafi jijini wakiungana na wanachama kutoka kwenye matawi yao yote huku pia kukiwa na mchezo wa mpira kati ya viongozi wa Yanga pamoja na timu ya wasanii utakao ambatana na burudani kutoka kwa wasanii wakubwa ambao watawatangaza hapo baadaye.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >